# KUCHUNGUZA TASWIRA YA MWANAMKE NA MBINU ZA KIFANI KATIKA MASHAIRI: MFANO WA DIWANI YA MIDULU

**FLORIAN AUGUST KIMARO**

**TASINIFU HII IMEWASILISHWA KAMA SHARTI PEKEE LA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2016**

# UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa anathibitisha kwamba amesoma Tasnifu hii iitwayo: **Kuchunguza Taswira ya Mwanamke na Mbinu za Kifani katika Mashairi: Mfano wa *Diwani ya Midulu*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

___________________________________

**Dr. Mohamed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

Tarehe: ____________________________

## HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Florian August Kimaro**, ninathibitisha kwamba tasnifu hii, iitwayo Kuchunguza Taswira ya Mwanamke katika Mashairi: Mfano wa *Diwani ya Midulu* ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa katika chuo chochote kwa lengo la kufuzu shahada yoyote.

…………………………………………

Sahihi

…………………………………………

Tarehe

# TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa familiya yangu ikiongozwa na mke wangu kipenzi Fransiska F. Kimaro, watoto wangu wapendwa; Benson F. Kimaro, Wilbard F. Kimaro na Innocent F. Kimaro. Pia, naitabaruku kazi hii kwa wadogo zangu Herment Kimaro, Venance Kimaro na Victor Kimaro.

## SHUKURANI

Awali ya yote, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema na mwenye Kurehemu. Mwenyezi Mungu andiye aliyenijaalia uhai na afya njema katika kipindi chote cha maisha yangu tangu kuzaliwa mpaka sasa. Wapo watu ambao tayari ameshawachukuwa mbele ya haki na wengine wapo katika hospitali kwa ajili ya matibabu lakini mimi nipo mzima wa afya tele. Ninasema asante sana ewe Baba Mwenyezi muweza wa kila jambo.

Shukurani zisizo kifani nazitoa kwa mwalimu wangu Dr. Mohamed Omary Maguo ambaye amejitahidi sana katika kunifunza na kuniongoza katika kuikamilisha kazi hii. Mwalimu alitumia muda mwingi katika kunielekeza lakini hakuchoka hata siku moja na zaidi alikuwa akinipa moyo kwamba nisikate tamaa kwani siku moja nitafanikiwa kumaliza. Malipo pekee ambayo ninaweza kumpatia mwalimu ni kumuombea mema katika maisha yake yote na Mwenyezi Mungu amjaalie aendelee kufanya kazi kwa hekima na busara.

Ninapenda pia, kutoa shukurani za dhati kwa familiya yangu yote kwa kuwa wavumilivu katika kipindi chote nilichokuwa masomoni. Muda mwingi walinikosa lakini walikuwa na imani kuwa nitamaliza masomo na kwenda kuungana nao tena. Namshukuru Mwenyezi Mungu nimefanikiwa kufikia hatua hii ambayo itaniwezesha kurudi nyumbani kukutana nao na kuendeleza maisha ya familiya yetu.

## IKISIRI

Utafiti huu ulizungukia lengo kuu ambalo lililenga kuchunguza taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*. Lengo kuu la utafiti huu lilikwenda sambamba na malengo mahususi matatu ambayo yalikuwa ni kubainisha taswira ya mwanamke katika mashairi ya Tigiti Sengo kama inavyosawiriwa katika *Diwani ya Midulu*, kuelezea sababu zilizofanya taswira ya mwanamke iwe hiyo inayosawiriwa katika *diwani hiyo* na kuchambua mbinu za kifani zilizotumiwa na mwandishi katika kujenga taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*. Malengo mahususi ya utafiti huu yameshughulikiwa ipasavyo baada ya kukusanya data za utafiti kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Data zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Ufeministi. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe mlezi, mwanamke na stara, mwanamke na kazi, uzuri wa mwanamke ni tabia na subira, mwanamke na uongozi na mwanamke na upendo. Sababu za mwanamke kusawiriwa hivyo ni kutokana na mafundisho ya dini, hali ya utandawazi, mabadiliko ya jamii kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Sababu hizi zimelezwa moja kwa moja katika uchambuzi wa data za lengo mahususi la kwanza kutokana na ukaribu wake kimaana. Vipengele vya mbinu za fani vilivyochambuliwa katika utafiti huu ni muundo wa takhmisa, tarbia na tathilitha, wahusika katika *Diwani ya Midulu*, mtindo; matumizi ya lugha ya kawaida, kiitikio na kibwagizo na matumizi ya lugha ya mafumbo.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........ **ii**

**HAKIMILIKI** ........ **iii**

**TAMKO LA MTAHINIWA** ........ **iv**

**TABARUKU** ........ **v**

**SHUKURANI** ........ **vi**

**IKISIRI** ........ **vii**

**SURA YA KWANZA** ........ **1**

**1.0 UTANGULIZI** ........ **1**

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 3

1.3 Tatizo la Utafiti ........ 6

1.4 Malengo ya Utafiti ........ 6

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti ........ 6

1.4.2 Malengo Mahususi ........ 7

1.5 Maswali ya Utafiti ........ 7

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 7

1.7 Mipaka ya Utafiti ........ 8

1.8 Mpangilio wa Tasinifu ........ 9

**SURA YA PILI** ........ **10**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** ........ **10**

2.1 Utangulizi ........ 10

2.2 Dhana ya Ushairi wa Kiswahili ........ 10

2.3 Taswira ya Mwanamke katika Mashairi .......... 13
2.4 Fani katika Ushairi .......... 21
2.5 Kazi Tangulizi kuhusu Mashairi ya Tigiti Sengo .......... 22
2.6 Mkabala wa Kinadharia .......... 23
2.6.1 Nadharia ya Ufeministi .......... 24
2.7 Hitimisho .......... 27
**SURA YA TATU .......... 29**
**3.0 MBINU ZA UTAFITI .......... 29**
3.1 Utangulizi .......... 29
3.2 Eneo la Utafiti .......... 29
3.3 Usanifu wa Utafiti .......... 29
3.4 Watafitiwa .......... 30
3.5 Sampuli na Usampulishaji .......... 30
3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa .......... 31
3.5.1 Data za Msingi .......... 31
3.7 Data za Upili .......... 31
3.8 Mbinu za Kukusanyia Data .......... 31
3.8.1 Usomaji Makini .......... 32
3.8.2 Upitiaji wa Nyaraka .......... 32
3.9 Uchambuzi wa Data .......... 33
3.10 Hitimisho .......... 33
**SURA YA NNE .......... 35**
**4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI .......... 35**

4.1 Utangulizi .......... 35

4.2 Taswira ya Mwanamke katika Diwani ya Midulu .......... 35

4.2.1 Mwanamke Kiumbe Mlezi .......... 36

4.2.2 Mwanamke na Stara .......... 39

4.2.3 Mwanamke na Kazi .......... 44

4.2.4 Uzuri wa Mwanamke Tabia na Subira .......... 48

4.2.5 Mwanamke na Uongozi .......... 51

4.2.6 Mwanamke na Upendo .......... 54

4.3 Matumizi ya Fani katika Diwani ya Midulu .......... 56

4.3.1 Kipengele cha Muundo katika Diwani ya Midulu .......... 57

4.3.2 Wahusika katika Diwani ya Midulu .......... 62

4.3.3 Kipengele cha Mtindo katika Diwani ya Midulu .......... 65

4.3.4 Matumizi ya Lugha ya Mafumbo .......... 72

4.3 Hitimisho .......... 73

**SURA YA TANO .......... 75**

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......... 75**

5.1 Utangulizi .......... 75

5.2 Muhtasari .......... 75

5.2.1 Taswira ya Mwanamke katika Diwani ya Midulu .......... 75

5.2.2 Sababu za Mwanamke Kusawiriwa Hivyo Alivyosawiriwa .......... 77

5.2.3 Matumizi ya Vipengele vya Kifani .......... 78

5.3 Hitimisho .......... 78

5.4 Mapendekezo .......... 79

**MAREJELEO .......... 80**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Utangulizi

Taswira ya mwanamke ni moja kati ya mambo yanayowavutia watafiti wa fasihi ya Kiswahili. Watafiti hao wamekuwa wakichunguza namna tanzu za ushairi, riwaya, tamthiliya, hadithi, semi na sanaa za maonesho zinavyomsawiri mwanamke katika maisha ya kila siku. Jambo kubwa linalowavutia watafiti katika kuchunguza taswira ya mwanamke ni kwamba inaaminika kuwa mwanamke amekuwa akipewa nafasi duni ikilinganishwa na mwanaume katika nyanja za elimu, kazi, uongozi, mirathi, kushiriki katika maamuzi na kupatiwa thamani inayostahiki.

Tigiti Shaaban Yusuph Mnyagatwa Kibwana Sengo ambaye ndiye mtunzi wa Diwani ya Midulu alizaliwa mwaka 1945 katika eneo la Kizuka katika shamba la mkonge Ngerengere. Alipata elimu yake ya msingi katika shule za Kidugalo, Ngerengere na Msamvu. Elimu ya sekondari aliipata katika shule za Mzumbe na Mazengo. Baada ya kufuzu elimu ya sekondari alijiunga na chuo cha ualimu cha Peramiho na kuhitimu mwaka 1968. Alipohitimu alifundisha katika shule na vyuo mbalimbali vya ualimu kabla ya kujiunga na elimu ya juu katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Alisoma shahada ya kwanza katika elimu na sanaa mnamo mwaka 1970 mpaka 1973. Baadae mwaka 1978-1985 alijiunga katika Chuo Kikuu Cha Khartoum kwa masomo ya uzamili na uzamivu.

Mwaka 1985 aliporudi kutoka Khartoum aliendelea kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1996 alipohamia katika Chuo Kikuu Cha Kiislamu Cha

Mbale nchini Uganda. Mwaka 2000 na kuendelea mpaka sasa anafanya kazi ya uhadhiri, utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Katika utafiti na uandishi wa vitabu amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutoa kazi nyingi za kitaaluma. Moja kati ya kazi hizo ambayo iliwahi kupata umaarufu sana enzi hizo ni ile ya *Hisi Zetu* na *Ndimi Zetu* alizoandika kwa pamoja na Saifu Kiango. Kazi hizi zilipata umaarufu mkubwa kutokana na kuandika mambo mazuri na vijana wadogo kitaaluma. Kazi hizi ni marejeleo ya kutumainiwa na wahakiki na watafiti wa masuala ya fasihi ya Kiswahili. Hivi karibuni amefanikiwa pia kutoa vitabu vingine vingi lakini katika utafiti huu tumeteua kitabu cha *Diwani ya Midulu* kwa lengo la kuchunguza taswira ya mwanamke. Hii ni Diwani ambayo inashughulikia masuala ya kawaida yahusuyo maisha ya kila siku ya jamii. Mashairi katika Diwani hii yametungwa kutokana na matukio ambayo yanakuwa yakitokea kila siku machoni mwa mwandishi na wakati mwingine kutokana na simulizi anazopata kutoka kwa watu wanaomzunguka. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kuwa hii ni diwani ya jamii na taswira ya mwanamke tunayoizungumzia ni sehemu ya mambo ya jamii.

Hivyo, katika utafiti huu tumechunguza taswira ya mwanamke katika mashairi ya Tigiti Sengo kupitia kazi yake ya *Diwani ya Midulu*. Ili kufanikisha azma ya utafiti huu katika sura hii ya kwanza ya utafiti, tumewasilisha vipengele vya usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu, malengo mahususi na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasinifu.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Usawiri wa taswira ya mwanamke katika kazi za fasihi ni dhamira kongwe inayojitokeza tangu pale fasihi ilipoanza kutumiwa na wanadamu kama chombo cha kutolea elimu, kutunza historia ya jamii, kuburudisha, kuonya, kufunza, kuadili na kuadibu. Utanzu wa kwanza kabisa katika ulimwengu wa fasihi ni ushairi ambao ndio pia ulioanza kumsawiri mwanamke katika hali tofautitofauti (Mulokozi, 1996). Kutokana na nafasi kubwa aliyonayo mwanamke katika mafanikio ya jamii, mwanamke anasawiriwa kwa mapana na marefu katika ushairi wa Kiswahili tangu enzi la ushairi simulizi na andishi pale tu maandishi yalipoanza kutumika (Harris, 1962). Mwanamke alitazamwa kama kiumbe ambaye ana uwezo mkubwa wa kuhakikisha kuwa maisha ya mwanaume na familia kwa jumla yanakuwa ni ya mafanikio makubwa (Mulokozi, 1975). Mfano mzuri ni mashairi ya Mwanakupona binti Mshamu yanayoeleza namna mwanamke anavyotakiwa kuishi katika maisha ya ndoa kwa kumheshimu na kumtii mumewe. Kumheshimu na kumtii mumewe ni mambo ya msingi mno ambayo yanamfanya mwanaume atulie kisaikolojia na kufanya kazi kwa utulivu, juhudi na maarifa ili kuiletea familia yake maendeleo. Inapotokea mwanamke akawa hamtii na kumheshimu mumewe, upo uwezekano wa mwanaume huyo kutotulia kisaikolojia na hatimaye kushindwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kwa kuwa muda mwingi atakuwa akifikiri juu ya tabia ya mkewe (Ramadhani, 2013).

Hata hivyo, taswira ya mwanamke inayoonekana katika mashairi ya Mwanakupona kupitia *Utenzi wa Mwanakupona* inatafsiriwa na wataalamu mbalimbali kuwa ni gandamizi kwa mwanamke ambapo anaonekana kama chombo cha starehe kwa

mwanaume. Katika utenzi huo mwanamke anachorwa kama kiumbe cha ndani, hatakiwi kutoka nyumbani bila ruhusa ya mumewe, ajipambe vizuri ili kumvutia mumewe, amkandekande mumewe ili kumtoa machovu, asipandishe sauti yake juu wakati anaongea na mumewe na mengine mengi zaidi ya haya (Khatib, 1985). Usawiri wa mwanamke katika hali kama hii umejitokeza pia katika kazi za mashairi ya watunzi wa miaka ya hivi karibuni kama Shaaban Robert katika kazi zake za *Ashiki Kitabu Hiki*, *Pambo* na hata *Mapenzi Bora*. Harris (1962) anasema kuwa, usawiri wa mwanamke katika hali kama ile ya *Utenzi wa Mwanakupona* inatokana na mafundisho ya dini ya Kiislamu na utamaduni wa Kiarabu. Mawazo haya yanaungwa mkono na Knappert (1977) pale anaposema kuwa maijilio ya Waarabu katika Pwani ya Afrika ya Mashariki kulileta athari kubwa katika ushairi wa Kiswahili. Utamaduni wa fasihi ya Kiaarabu na dini ya Kiislamu uliofundishwa na wageni hao ulifanya sehemu ya dhamira muhimu katika kazi za fasihi ukiwemo ushairi wa Kiswahili. Wazo hili tunakubaliana nalo kwamba ni ukweli uliowazi kwamba Waarabu walikuja katika Pwani ya Afrika ya Mashariki mnamo karne ya 7 kwa malengo ya kufanya biashara na kueneza dini pamoja na utamaduni wa Kiarabu (Mulokozi na Sengo, 1995). Katika harakati zao walifanikiwa kwa kiasi kikubwa kufanya utamaduni wa jamii ya Waswahili wa Pwani kufanana na ule wa Kiarabu na kuleta athari katika dhamira za mashairi na tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili (Knappert, 1977).

Wataamu mbalimbali wa ushairi wa Kiswahili wanadai kuwa dini ya Kiislamu na utamaduni wa Kiarabu ndio uliosababisha mwanamke kusawiriwa katika hali ya kumtumikia mwanaume na kuwa kama chombo chake cha starehe. Sengo (2009)

anapingana na mawazo haya ambapo yeye anaona kuwa suala la mwanamke kusawiriwa kama anavyosawiriwa katika kazi za ushairi ni jambo la asili na hakuna mtu anayeweza kupingana nalo. Anaeleza kuwa maumbile ya mwanamke yanamtaka kufanya mambo ambayo yanaendana na uanamke wake ambayo ni kupika chakula, kulea watoto, kumlea mume na kumstarehesha, kusafisha nyumba, kufua nguo, kuosha vyombo na kuwalea na kuwathamini ndugu wa mume.

Mtaalamu huyu anaonya kuwa isije ikachukuliwa kwamba, mwanamke kuyafanya mambo haya ni kuonewa na kudunishwa la hasha bali itazamwe kuwa hii ni heshima kubwa kwa mwanamke katika kuijenga na kuiendeleza familia na jamii kwa jumla. Mwanamke ni kiumbe mwenye nguvu na uwezo mkubwa wa kuitumikia jamii hata kuliko mwanaume (Sengo, 2009). Hii inatokana na uthibitisho wa mambo yanayofanywa na mwanamke kuwa ni mengi ikilinganishwa na kazi anazofanya mwanaume.

Sengo (2009) anawaona wataalamu wanaolaumu mwanamke kusawiriwa kama anavyosawiriwa katika kazi za ushairi kama *Utenzi wa Mwanakupona* kuwa wanakosea na hawajui kwamba ni sahihi mwanamke kusawiriwa hivyo. Mtaalamu huyu anadai kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye vyeo takribani nane ambavyo ni mama, dada, shemegi, shangazi, mkwe, mama mkwe, binti na bibi au nyanya. Vyeo vyote hivi vinaashiria nafasi aliyonayo mwanamke katika jamii kwamba ni kubwa kuliko ya mwanaume. Ni kutokana na msimamo wa mwandishi huyu ndipo tukaona ipo haja ya kutafiti taswira ya mwanamke katika kazi yake ya *Diwani ya Midulu* ili kuona yeye anamsawiri vipi mwanamke?

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Taswira ya mwanamke katika kazi za ushairi inajitokeza katika mikondo miwili ambayo ni mkondo wa hali hasi na mkondo wa hali chanya. Usawiri wa taswira hii umekuwa hivyo tangu enzi na enzi ambapo mkondo wa uhasi ndio unaoonekana kuwa mkubwa zaidi kuliko mkondo wa uchanya (Sengo, 2009). Wataalamu kadhaa wamefanya utafiti wa kuchunguza taswira ya mwanamke katika ushairi na kutoa mahitimisho yanayoonesha kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe duni ambaye ameumbwa na Mungu kwa lengo la kumstarehesha mwanaume hapa duniani. Wataalamu hao ni Omary (2008), Samwel (2010), Ramadhani (2013), Kahalifa (2013) na Ali (2014). Wataalamu hawa wanaonesha kuwa miongoni mwa mambo anayosawiriwa nayo mwanamke kuwa yeye ni kiumbe tegemezi kwa mwanaume na kutokana na utegemezi huo ni lazima afanye mambo ya kumridhisha mwanaume. Sengo (2009) kama tulivoona mawazo yake kuhusiana na suala hili ni kuwa si kweli kwamba mambo anayoyafanya mwanamke juu ya mwanaume yanamfanya aonekane ni duni mbele ya mwanaume. Kutokana na mawazo haya ndipo tulipopata ari ya kutafiti kazi zake za ushairi ili kuona yeye anamchora vipi mwanamke? Hivyo, katika utafiti huu tumechunguza taswira ya mwanamke katika mashairi ya Tigiti Sengo kupitia kazi yake ya *Diwani ya Midulu*.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahususi matatu kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza taswira ya mwanamke na Mbinu za Kifani

zilizotumika katika *Diwani ya Midulu*.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni:

i) Kubainisha taswira ya mwanamke katika mashairi ya Tigiti Sengo kama inavyosawiriwa katika *Diwani ya Midulu*.

ii) Kuelezea sababu zinazofanya taswira ya mwanamke iwe hiyo inayosawiriwa *katika Diwani ya Midulu*.

iii) Kuchambua mbinu za kifani zilizotumiwa na mwandishi katika kujenga taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i) Taswira ya mwanamke inajitokezaje katika *Diwani ya Midulu*?

ii) Ni sababu zipi zinazofanya mwanamke asawiriwe hivyo anavyosawiriwa katika *Diwani ya Midulu*?

iii) Ni mbinu gani za kifani zilizotumika katika kujenga taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu katika kukuza taaluma ya ushairi wa Kiswahili kwa namna mbalimbali. Kwanza kabisa utafiti huu utakuwa ni rejeleo muhimu kwa wahadhiri na wanafunzi wanaosoma fasihi ya Kiswahili na hususani ushairi wa Kiswahili katika ngazi mbalimbali za taaluma ya ushairi. Wahadhiri watautumia utafiti huu kama rejeleo katika kuandaa maalumati ya masomo kabla ya kwenda

darasani kutoa muhadhara. Sambamba na hilo pia watautumia utafiti huu kama rejeleo katika kuandika vitabu na makala za kitaaluma kwa nia ya kukuza fasihi ya Kiswahili.

Wanafunzi kwa upande wao watautumia utafiti huu kama rejeleo muhimu katika kujisomea wakitafuta pengo la maarifa la kulifanyia utafiti. Kwa kuusoma utafiti huu, wanafunzi wataweza kupanua uelewa wao zaidi na kufanikiwa kubaini maeneo mapya ya kufanyia utafiti. Kwa wanafunzi watakaovutiwa na mapendekezo ya utafiti huu yatakayotolewa katika sura ya tano ya tasinifu itakapokamilika watanufaika na maeneo ya utafiti zaidi tutakayoyapendekeza.

Utafiti huu pia utakuwa na umuhimu mkubwa kwa jamii nzima kwa ujumla wake kwa sababu mambo yatakayochambuliwa na kuwasilishwa katika tasinifu yanahusu jamii yenyewe. Wanaharakati wa masuala ya jinsia watauona utafiti huu kuwa na umuhimu mkubwa katika kufanikisha harakati zao za kumkomboa mwanamke. Matokeo ya utafiti huu yatawasaidia katika kuandaa mikakati na programu za kuleta usawa wa kijinsia katika jamii.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kushughulikia taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*. Baadhi ya taswira hizo ni: Mwanamke na Stara,Mwanamke na Kazi, Uzuri wa Mwanamke tabia na subira, Mwanamke na Uongozi,Mwanamke na Upendo na Mwanamke Kiumbe Mlezi. Katika diwani hii kunaelezwa mambo mengi lakini sisi tumejikita katika kuchunguza taswira ya mwanamke katika kazi hizi za mtunzi nguli

wa fasihi ya Kiswahili. Katika kuchunguza taswira ya mwanamke pia tumeangazia sababu zilizofanya mwanamke asawiriwe hivyo alivyosawiriwa na kisha tumewasilisha mbinu za kifani zilizotumika katika kujenga taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*.

## 1.8 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu ya utafiti huu imeandikwa katika mpangilio wa sura tano. Sura hizo ni sura ya kwanza inayokuwa na masuala ya kiutangulizi kama vile, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Sura ya pili imewasilisha mapitio ya kazi tangulizi kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali na sura ya tatu imewasilisha mbinu za utafiti. Sura ya nne imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti na sura ya tano imetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadae.

# SURA YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumefanya mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia ambapo tumeweza kutoa ithibati ya kufanyika kwa utafiti huu. Babbie (1999) anaeleza mapitio ya kazi tangulizi hufanywa ili kubaini watafiti watangulizi wameshughulikia jambo gani mpaka hivi sasa na jambo gani bado hawajashughulikia. Kwa maneno mengine ni sawa na kusema kuwa, mapitio ya kazi tangulizi ndiyo yanayobainisha pengo la utafiti. Yaliyopitiwa katika sura hii ni pamoja na utafiti wa nafasi ya mwanamke katika ushairi, kazi tangulizi zinazohusu kazi za Tigiti Sengo na mkabala wa kinadharia.

### 2.2 Dhana ya Ushairi wa Kiswahili

Ushairi wa Kiswahili umejadiliwa na wataalamu tafautitafauti kwa nia na malengo yaliyolenga kukamilisha mitazamo na misimamo yao. Dhanna ya Ushairi wa Kiswahili imejadiliwa kwa mashiko na hamasa kubwa katika miaka ya 1970 ikihusishwa na ulioitwa mgogoro wa Ushairi wa Kiswahili (Mayoka, 1984). Wapo waliodai kuwa ushairi wa Kiswahili asili yake ni fasihi ya Kiarabu na Dini ya Kiislamu (Harris, 1962) na wengine wakaeleza kuwa asili ya ushairi wa Kiswahili ni Nyimbo na Ngoma za Makabila ya Kiafrika (Mulokozi na Sengo, 1995). Kwa hali hiyo, kila kundi lina vigezo vyake na kutokana na vigezo hivyo ndipo wanaweza kueleza maana ya ushairi wa Kiswahili. Kwa kuwa si nia yetu kufafanua na kueleza kwa undani kuhusu mgogoro wa ushairi ni vema sasa tueleze maana ya ushairi kama

unavyoelezwa na wataalamu wa fasihi ya Kiswahili.

Abdilatif Abdalla kama anavyonukuliwa na Massamba (1983:57) anaeleza kuwa utungo ufaao kupewa jina la ushairi si utungo wowote bali ni utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinganifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye, wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizo pungufu wala zilizo zaidi. Na vipande hivyo viwe vimetandwa na maneno ya mkato maalumu na yenye lugha nyoofu, tamu na laini. Lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kusema, tumbuizi kwa masikio ya kuusikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ilivyokusudiwa.

Naye Mayoka (1984) anaeleza kuwa ushairi ni mtungo wa kisanaa ulio na mpangilio maalumu na lugha ya mkato ambayo ndani yake ina vina, urari wa mizani na muwala maalumu ambavyo kwa pamoja huwa na fani na maudhui yahusuyo hisi fulani au tukio juu ya maisha ya mtu au watu wa mazingira na wakati maalumu.

Fasili za ushairi zinazotolewa na wataalamu hawa wawili zinaonekana kukaribiana kimantiki hasa pale zinaposisitiza kuwa ushairi ni utungo wenye vina na mizani. Ikitokea utungo unaoitwa kuwa ni ushairi halafu hauna vina na mizani basi hauwezi kuitwa ushairi kamwe. Vile vile, wataalamu hawa wanasisitiza kuwa ushairi ni lazima uwe na muwala yaani msitari wa kwanza wa shairi uwe na uwiano wa kimaana na msitari unaofuata na hatimaye beti zote kuwa na muwala. Mawazo ya wawili hawa kuhusu maana ya ushairi ni muhimu mno katika kufanikisha malengo ya utafiti wetu. Katika utafiti wetu tumechunguza pia fani katika kitabu cha *Diwani*

*ya Midulu*. Hivyo, tunakumbushwa kuwa miongoni mwa vipengele muhimu vya kutazama na kushughulikia katika fani ya mashairi ni vina na mizani ambavyo bila shaka yoyote kutumika kwake kuna dhima maalumu.

Sambamba na hilo, wataalamu hawo wanaoeleza kuwa ushairi ni lazima uwe na matumizi ya lugha ya mkato na mnato ambayo ni telezi kwa ulimi wa kuitamka na laini kwa masikio ya kuisikia. Jambo hili ni muhimu sana katika kuutafautisha ushairi na tungo nyingine. Hii ni kwa sababu ushairi hueleza mambo kwa maneno machache na hivyo kuwa na lugha ambayo ni tamu huufanya ushairi kueleza mambo mengi kwa ufupi. Pia, lugha ya mashairi humfanya msomaji kuvutika zaidi katika kusoma au kusikiliza shairi lililopelekwa mbele yake. Mawazo haya yana nafasi muhimu katika kuukamilisha utafiti wetu kwani umetufahamisha moja kati ya vipengele muhimu vya fani ambavyo tutavitafiti katika utafiti tuanaoukusudia kuufanya. Sambamba na hilo, kwa maoni yetu tunaona kuwa, ushairi ni lazima uwe na matumizi ya lugha ya mnato ambayo ni laini na tamu kwa masikio yenye kusikiliza na telezi kwa ulimi wenye kutamka ni ya jumla mno. Hii inatokana na ufahamu wetu kuwa si kila msomaji au msikilizaji anaweza kuwa na hisia inayofanana na wengine juu ya lugha ya mashairi. Lugha ambayo ni tamu na laini kwa mtu mmoja haiwezi kuwa tamu na laini kwa mtu mwingine na kadhalika.

Kimsingi, fasili mbili za maana ya ushairi zilizotolewa hapo juu ni kwa mujibu wa wanamapokeo na sasa tutazame wanausasa nao wanasema nini. Kwa upande wao Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha yenye muwala, kwa lugha ya mkato,

picha, au sitiara, au ishara, katika usemi, maandishi, au mahadhi ya wimbo, ili kuelekeza wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu, kwa njia inayogusa moyo.

Jambo kuu linaloitafautisha fasili hii na ile inayotolewa na wanamapokeo ni kuwa hii haitilii manani kuwa vina na mizani ni sehemu ya ushairi. Ushairi siyo lazima uwe na vina na mizani ndiyo uitwe ushairi. Kwao shairi linaweza kuwa na muundo au mtindo wowote ule na bado likaendelea kuwa ni shairi. Sambamba na hilo, wanaonekana kukubaliana na wanamapokeo kuhusu lugha ya ushairi. Wao wanausasa wanasema kuwa shairi linapaswa kuwa na lugha ya mkato, picha, ishara na sitiari mambo ambayo pia yanasisitizwa na wanamapokeo. Kwa hiyo, makundi yote mawili yanakubaliana kuwa ni lazima shairi liwe na matumizi ya lugha ambayo yatamvuta msomaji kusoma zaidi na msikilizaji kusikiliza kwa makini zaidi. Mashairi ya Tigiti Sengo kupitia katika *Diwani ya Midulu* na *Tungizi za Mnyagatwa* yana sifa zote muhimu ambazo zinaunda ushairi wa Kiswahili. Hivyo katika utafiti huu tumechunguza taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*.

## 2.3 Taswira ya Mwanamke katika Mashairi

Kazi tangulizi kuhusiana na taswira ya mwanamke katika mashairi ya Kiswahili zimefanywa na wataalamu mbalimbali (Ali, 2014). Miongoni mwa walioandika kuhusu taswira ya mwanamke katika mashairi ya Kiswahili ni Kitogo (2002). Katika utafiti wake alizungumzia juu ya mchango wa mashairi ya Saadani Kandoro katika kukuza na kuendeleza siasa nchini Tanzania. Moja kati ya mambo aliyoyabaini ni kuwa mashairi ya Saadan Kandoro yanamsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye

nafasi kubwa katika kusaidia jitihada za kufanikisha siasa za Azimio la Arusha la mwaka 1967. Hili linabainika pale anapoonesha kuwa kufanikiwa kwa siasa za ujamaa na kujitegemea ni umoja ambao unapaswa kufanywa na watu wote wakiwemo wanaume na wanawake katika jamii. Jambo hili tunakubalina nalo kwa asilimia nyingi kwa sababu ni kweli kwamba jamii inapoungana kwa pamoja juu ya jambo lolote lile basi jambo hilo ni lazima lifanikiwe. Mawazo haya tumeyachukuwa na tumetazama ni kwa vipi yanajitokeza katika mashairi ya *Diwani ya Midulu*.

Pamoja na maelezo mazuri juu ya taswira ya mwanamke katika mashairi ya Saadan Kandoro lakini kunatokea taswira hasi ya mwanamke katika mashairi hayo. Katika moja ya mashairi ya mwanamke Saadan anawahimiza wanajamii kufanya kila linalowezekana ili kujikomboa kutoka katika mikono ya wakoloni. Katika kufanya hivyo, anatoa msisitizo kwamba "ni mume si mke ndiye anaweza kufanya mapinduzi katika jamii." Kauli hii inatoa taswira hasi ya mwanamke katika jamii kwamba ni wanaume pekee ndio wenye uwezo wa kufanya mambo mbalimbali ya kukomboa jamii zao jambo ambalo si kweli. Mawazo haya hatukubaliani nayo kwa sababu tunaamini kuwa mwanamke anao mchango mkubwa katika ukombozi wa jamii. Hata hivyo, mawazo haya tumeyachukuwa na tumeyafanyia kazi katika kutazama ni kwa vipi taswira ya mwanamke kuhusiana na ukombozi inajitokeza katika mashairi ya *Diwani ya Midulu*.

Frolova (2003) aliandika makala aliyoipa jina la, "Euphrase Kezilahabi the Renewal of Kiswahili Poetry." Katika makala haya anasisitiza kwamba miongoni mwa mambo yanayofanya amuite Kezilahabi kuwa ni muhuishaji wa ushairi wa Kiswahili

ni kwamba anatumia sana lugha ya picha, ishara na taswira katika kuelezea masuala mbalimbali yanayohusu jamii yakiwemo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Matumizi ya lugha ya aina hii yanafanya kazi za mashairi za Kezilahabi kuonekana kuwa ni ngumu na hazieleweki kwa urahisi kwa wasomaji wake. Tunakubaliana na mawazo haya na tunakiri kwamba ni kweli matumizi ya lugha ya picha, ishara na taswira katika kazi za Kezilahabi yanafanya kazi hizo kutoeleweka kwa wasomaji. Hata hivyo, matumizi ya lugha ya namna hii husaidia katika kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa wasomaji ikiwemo nafasi ya mwanamke katika jamii. Mawazo haya tumeyachukua na tumeyafanyia kazi katika utafiti wetu kwamba tumekuwa makini katika kutazama lugha ya picha na ishara inavyosaidia kujenga taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*.

Mwanamke anasawiriwa kama mama mlezi katika jamii kupitia mashairi ya bongo fleva (Omari, 2008). Mwanamke anasawiriwa kama mtu muhimu katika kurithisha maadili kwa watoto kutoka kizazi kimoja mpaka kingine. Akitolea mfano wimbo wa “Mama Yangu,” wa msanii Banana Zoro anasema kuwa wimbo huu umetumia lugha ya sitiari kusisitiza nafasi ya mama katika malezi ya watoto. Kwa mfano, sehemu ya wimbo huu inasema, “mama yangu, wewe ni nguzo maishani mwangu, ni taa imulikayo mbele yangu, daima milele aaah,” sitiari zinazomfananisha mwanamke sawa sawa na nguzo na taa. Mawazo haya tunakubaliana nayo na kwamba ni kweli mwanamke ni sawa sawa na nguzo na taa kwa sababu yeye ndiye anayekaa na watoto muda mrefu kuliko baba. Kutokana na hali hiyo anayo nafasi kubwa ya kuwapa watoto malezi mema au mabaya. Katika utafiti wetu tumechunguza ni nafasi ya mwanamke katika malezi ya watoto kupitia mashairi ya *Diwani ya Midulu*.

Omari (2009) alifanya utafiti na kuandika tasinifu yenye mada isemayo, "Bongo Fleva asa Popular Literature." Hii ni kazi iliyochunguza nyimbo za bongo fleva kama fasihi pendwa ya Kiswahili. Mtafiti alibaini kuwa bongo fleva ni fasihi pendwa na mambo ambayo yanaifanya kuwa fasihi pendwa ni kule kuzungumzia masuala yanayohusu mapenzi baina ya mwanamke na mwanaume. Katika upendwa huo mwanamke anachorwa kama kiumbe aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumstarehesha mwanaume kwa kumkidhia haja zake za kingono. Mawazo haya tunakubaliana nayo kwa sababu bongo fleva ni nyimbo za vijana na dhamira kubwa ya vijana katika maisha ni suala la mapenzi. Hivyo, kuzungumzia mapenzi katika nyimbo za bongo fleva ni jambo la kawaida kwa vijana lakini ni jambo la ajabu kwa watu wa makamu na wazee katika jamii. Katika utafiti wetu tumechunguza kama mwandishi wa mashairi ya *Diwani ya Midulu* anamsawiri mwanamke kama hivi anavyosawiriwa katika mashairi ya nyimbo za bongo fleva.

Ismaili (2010) aliandika makala juu ya "bongo fleva katika kuelimisha jamii juu ya masuala ya haki katika jamii." Katika makala yake haya anabainisha kuwa nyimbo za bongo fleva zina nafasi kubwa katika kuelimisha wanajamii juu ya haki zao za msingi zikiwemo za kupata elimu, huduma ya afya, maji, umeme na miundo mbinu bora ya usafirishaji. Anatolea mfano, nyimbo za Joseph Haule maarufu kama Profesa Jay wa "Ndiyo Mzee na Siyo Mzee," anaeleza kuwa nyimbo hizi zinatumika katika kuwaelimisha wananchi katika kufahamu haki zao za msingi katika masuala ya uchanguzi wa kidemokrasia. Kupitia nyimbo hizi wananchi wanatakiwa kufahamu kuwa wao ndio wenye haki ya kumchagua au kutomchagua mtu yeyote na kumpa nafasi ya kuongoza katika jamii.

Mawazo haya ni sahihi na tunakubaliana nayo kwa asilimia nyingi. Katika chaguzi za kidemokrasia ni haki ya wananchi kuwachagua viongozi na kuwapa mamlaka ya kuongoza kwa kipindi fulani kulingana na katiba ya nchi hiyo. Mawazo haya yametufamisha pia katika masuala ya haki za wananchi mara nyingi wanawake huwekwa nyuma na hasa katika masuala ya siasa. Wanawake huonekana kuwa ni watu wa kupiga kura tu lakini wao huwa nyuma katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi. Katika utafiti wetu tumeonesha namna wanawake katika *Diwani ya Midulu* wanavyohimizwa katika kudai haki zao ikiwemo ile ya kugombea nafasi za uongozi.

Mwanamke anasawiriwa kama chombo cha starehe kwa mwanaume kupitia nyimbo za bongo fleva (Samwel, 2010). Katika makala yake (Samwel, 2010) anaeleza kuwa karibu asilimia 90 ya nyimbo za bongo fleva zinazungumzia mapenzi katika jamii na hasa mapenzi ya mwanamke na mwanaume. Katika dhamira hiyo ya mapenzi mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye anapenda starehe na anasa kiasi cha kupenda fedha na hivyo kutumiwa na wanaume kama chombo cha starehe. Haya yanathibitishwa na uvaaji wa nguo wa wanawake katika unenguaji majukwaani katika maonesho ya nyimbo za bongo fleva na hata katika muziki wa dansi. Baadhi ya wanaume huvutiwa sana na mavazi ya wanawake waliovaa nusu uchi kuwa ni kama kiburudisho kwao. Mawazo haya tunakubaliana nayo kwa asilimia mia moja kwamba ni kweli taswira ya mwanamke katika nyimbo za bongo fleva ni kwamba mwanamke anasawiriwa kama chombo cha starehe. Katika utafiti wetu tumechunguza kwa lengo la kubaini kama mwanamke anasawiriwa kama chombo cha starehe katika mashairi ya *Diwani ya Midulu*.

"Masuala ya kisiasa katika Mashairi ya Euphrase Kezilahabi: Uchunguzi kifani wa diwani za *Karibu Ndani* na *Dhifa*," ni tasinifu ya shahada ya Uzamili iliyoandikwa na Omary (2011). Katika tasinifu hii kumeelezwa masuala mbalimbali ya kisiasa lakini mojawapo ni nafasi ya mwanamke katika jamii. Kezilahabi anamsawiri mwanamke kama kiumbe ambaye anastahili kupatiwa elimu ya kutosha ili aweze kutoa mchango wake katika maendeleo ya jamii. Taswira hii ya mwanamke inajitokeza katika shairi la "Binti," lililopo katika diwani ya *Dhifa* ambapo mwanamke anatakiwa kutokukubali kudanganywa na maneno ya wanaume kuwa anapendwa na kuacha kusoma kwa juhudi na maarifa katika masomo yake. Mawazo haya tunakubaliana nayo kwani ukweli usiopingika kwamba baadhi ya wasichana huacha shule baada ya kudanganywa na kupewa ujauzito. Mwanamke anayepewa ujauzito akiwa masomoni hasa katika ngazi ya shule ya msingi na sekondari hupoteza ndoto zake za kuwa msomi mzuri mwenye maarifa yatakayosaidia kuleta maendeleo katika jamii yake. Katika utafiti wetu tumechunguza namna mashairi ya *Diwani ya Midulu* yanavyomsawiri mwanamke kama kiumbe ambaye anatakiwa kupata elimu ya kutosha kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa jamii yake.

Alhabib (2012) aliandika tasinifu ya shahada ya uzamili ikiwa na anuani isemayo, "Taswira katika nyimbo za Taarab." Katika utafiti wake huu aligundua kuwa mwanamke anasawiriwa katika taswira mbalimbali zikiwemo, mwanamke ni mama, mlezi, mvumilivu, malaya, muovu, mbeya, mfitinishaji, muongo na msaliti. Tukiangalia kwa harakaharaka tunabaini kuwa mwanamke anasawiriwa katika hali hasi zaidi kuliko hali chanya. Mawazo haya tunakubaliana nayo kwa sababu watafiti wengi watangulizi wanakubaliana kwamba mwanamke anasawiriwa katika hali hasi

kwa kiasi kikubwa kuliko hali chanya. Mawazo haya yametusaidia katika uchambuzi wa data za utafiti wetu kwani pia tumejaribu kutazama katika mashairi ya *Diwani ya Midulu* mwanamke anasawiriwa zaidi katika hali gani kati ya chanya na hasi?

Khalifa (2013) alifanya utafiti na kuandika tasinifu ya shahada ya uzamili juu ya "masuala ya kijinsia katika nyimbo za bongo fleva." Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa mwanamke anasawiriwa katika hali hasi kwa kiasi kikubwa huku mwanaume akisawiriwa katika hali chanya kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, mwanamke anasawiriwa kama kiumbe muovu ambaye anasababisha kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI katika jamii huku mwanaume akisawiriwa kama kiumbe mwenye akili na uwezo wa kuzalisha mali kwa ajili ya matumizi ya familia yake. Kwa hakika mawazo haya hayana ukweli kwani suala la kuambukiza UKIMWI ni la wote, wanawake na wanaume kwa sababu njia kuu ya maambukizi ni ngono kitendo kinachofanywa kwa pamoja baina ya mwanaume na mwanamke. Katika utafiti wetu tumechunguza kama katika mashairi ya *Diwani ya Midulu* mwanamke anasawiriwa kama kiumbe muovu anayesababisha matatizo katika jamii.

Kombo (2014) alichunguza mashairi ya magazetini yanayozungumzia masuala ya UKIMWI na athari zake katika jamii. Katika utafiti wake alibaini kwamba, mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye ni chanzo cha ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Mwanamke anasawiriwa katika mashairi mengi ya magazetini kama kiumbe ambaye ni malaya na kutokana na umalaya wake ndio maana UKIMWI umeenea kwa kasi kubwa katika jamii ya Watanzania na katika nchi nyingine za Afrika. Mawazo haya ni ya kweli kwani jamii humtazama mwanamke kama kiumbe

ambaye ni malaya na kutokana na umalaya huo jamii inateseka na maambukizo ya ugonjwa hatari wa UKIMWI. Kwa hakika, jambo hili halina ukweli wowote kwani umala ni tabia ya mtu na wote mwanamke na mwanaume wanaweza kuwa malaya. Hakuna mwanamke anayeweza kufanya umalaya yeye mwenyewe bila ya kuwepo mwanaume wa kufanya naye umalaya. Hivyo, si sahihi kumlaumu mwanamke kwamba yeye ndiye anayesababisha kuongezeka kwa maambukizi ya UKIMWI bali hata wanaume pia wanastahili kulaumiwa. Katika utafiti wetu tumechunguza kama mwanamke anasawiriwa katika *Diwani ya Midulu* kwa kulaumiwa kuwa yeye ndiye chanzo cha maambukizi ya UKIMWI katika jamii.

Ali (2014) alifanya utafiti na kuandika tasinifu iliyolinganisha usawiri wa mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Katika utafiti huu alibainisha kuwa washairi hawa wawili wanafanana sana kuliko wanavyotofautiana katika kumsawiri mwanamke katika mashairi yao. Wamejitahidi sana katika kumsawiri mwanamke katika hali chanya lakini wamefika mahali wameshindwa na wakajikuta wanamsawiri mwanamke katika hali hasi. Swali la msingi tulilojiuliza ni kuwa, ni kwa nini washairi hawa wameshindwa kumsawiri mwanamke katika hali chanya tu kama walivyokuwa wamekusudia. Kwa haraka haraka tumepata jawabu kwamba katika jamii kuna mfumo dume ambao ndio unaofanya mwanamke asawiriwe hivyo anavyosawiriwa kwa kuwa ni vigumu kwa mtunzi kukwepa hali halisi ya maisha. Katika utafiti huu tumechunguza mchango wa mfumo dume katika ujengaji wa taswira ya mwanamke katika mashairi ya *Diwani ya Midulu*.

## 2.4 Fani katika Ushairi

Khalifani (2013) alifanya utafiti uliokuwa na lengo la kuchunguza masuala ya kisiasa katika mashairi ya Saadani Kandoro. Miongoni mwa masuala ya kisiasa yaliyoainishwa na mtafiti huyu kuwa yanatokeza katika mashairi ya Saadan Kandoro ni pamoja na uongozi mbaya katika jamii, masuala ya haki, umuhimu wa elimu, huduma za afya, ujamaa na kujitegemea, usawa wa kijinsia na umoja na mshikamano katika jamii. Utafiti huu umekuwa na mchango mkubwa katika kuwezesha kukamilika kwa utafiti wetu kutokana na kule kutuainishia baadhi ya mambo ambayo tunayahitaji katika utafiti wetu. Mambo hayo ni masuala ya jinsia ambapo wanawake hawapewi fursa sawa na wanaume katika nafasi za maamuzi katika jamii. Katika utafiti wetu tumechunguza ni namna gani mashairi ya *Diwani ya Midulu* yanahamasisha upatikanaji wa fursa sawa kwa jinsia zote katika jamii.

Mansour (2013) alifanya utafiti uliolinganisha matumizi ya lugha baina ya mashairi ya kimapokeo na kisasa kwa kurejelea mashairi ya Haji Gora Haji na Euphrase Kezilahabi. Haji Gora Haji ni mshairi anayetunga mashairi yenye kufuata urari wa vina na mizani na Euphrase Kezilahabi anatunga mashairi yasiyofuata urari wa vina na mizani. Matokeo ya utafiti wake huo yanaonesha kuwa kazi za waandishi hao ambazo ni *Kimbunga* ya Haji Gora Haji na *Dhifa* ya Kezilahabi zinatofautiana sana hasa katika suala la urari wa vina na mizani. Lakini kwa upande wa matumizi ya lugha ya mafumbo, mashairi ya wawili hawa yanafanana na hata baadhi ya dhamira zinazoelezwa katika mashairi hayo zinafanana sana. Ingawa kazi hii haikuwa na malengo yanayofanana na ya utafiti wetu lakini umetusaidia kutambua kuwa matumizi ya lugha ya mafumbo ni muhimu sana katika kuwasilisha dhamira za

mashairi kwa hadhira iliyokusudiwa. Katika utafiti wetu tumechunguza namna matumizi ya lugha yalivyosaidia katika kujenga taswira ya mwanamke katika mashairi ya *Diwani ya Midulu*.

Kombo (2014) alifanya utafiti uliolenga kuchunguza matumizi ya lugha katika mashairi ya magazetini huku akirejelea mashairi yanayozungumzia ugonjwa hatari wa UKIMWI. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa miongoni mwa vipengele vya matumizi ya lugha vinavyojitokeza katika mashairi hayo ni tashibiha, tashihisi, sitiari, taswira na ishara. Kupitia matumizi haya ya lugha, dhamira mbalimbali kama vile unyanyapaa wa wagonjwa wa UKIMWI, asili na chimbuko la UKIMWI, athari ya UKIMWI kwa jamii na masula ya UKIMWI na ukahaba yamewasilishwa vizuri kwa wasomaji wa mashairi hayo. Utafiti huu umetusaidia kuelewa mchango wa matumizi ya lugha katika kujenga dhamira nasi tumeweza kubaini ni kwa vipi matumizi ya lugha yamesaidia katika kujenga taswira ya mwanamke.

## 2.5 Kazi Tangulizi kuhusu Mashairi ya Tigiti Sengo

Kazi tangulizi juu ya mashairi ya Tigiti Sengo hazijafanywa kwa kiasi kikubwa kwa sababu mashairi yake ni mapya. Hata hivyo wapo baadhi ya wataalamu wametaja mashairi ya Tigiti Sengo katika harakati za kukamilisha utafiti wao au kutokana na kuvutiwa na kazi hizo. Miongoni mwao ni Safari (2010) alipoandika utangulizi katika *Diwani ya Midulu* na kueleza kuwa mashairi yaliyopo katika diwani hii ni hazina kubwa kwa taifa kwani ina mashairi mengi yenye kuelimisha lakini wakati huohuo yanaburudisha. Mashairi yaliyopo katika diwani hii yanazungumzia maisha ya kila siku ya jamii likiwemo suala na nafasi ya mwanamke katika jamii. Maelezo

haya tunakubaliana nayo kwa asilimia zote na kwamba katika utafiti wetu tumechunguza namna taswira ya mwanamke inavyojitokeza katika mashairi ya *Diwani ya Midulu*.

Omary (2015) aliandika tasinifu ya shahada ya Uzamivu akichunguza ufasihi simulizi katika mashairi ya Euphrase Kezilahabi ambaye ni mwandishi wa mashairi ya kisasa. Katika utafiti wake alibainisha kuwa mashairi ya Kezilahabi yameandikwa bila kufuata kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo kama ilivyo kwa mengi ya mashairi yanayopatikana katika kazi za watunzi wa mashairi ya Kiswahili akiwemo Tigiti Sengo. Tumeona katika maelezo haya kukitajwa kazi za Tigiti Sengo na bila shaka ni *Diwani ya Midulu* ambayo sisi tumeishughulikia kwa mawanda mapana zaidi. Mtaalamu huyu aliishia katika kuzitaja tu kazi za ushairi za Tigiti Sengo lakini katika utafiti huu tumechambua taswira ya mwanamke katika mashairi ya *Diwani ya Midulu*.

## 2.6 Mkabala wa Kinadharia

Katika kazi za taaluma mbalimbali matumizi ya nadharia huwa ni kitu cha msingi katika kuthibitisha ukweli wa kitu au jambo fulani. Cresswell (2009) anaeleza kuwa nadharia ni istilahi ya kiujumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi za fasihi kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Cresswell (ameshatajwa) anaendelea kueleza kuwa nadharia ni mawazo au maelezo ya jambo ambayo hufungamana na vigezo vilivyowekwa na jopo la wataalamu au mtu binafsi. Msomaji wa kazi ya fasihi anapaswa kuelewa mawazo au vigezo hivyo vitakavyomuwezesha kuisoma kazi ya fasihi kwa utaratibu maalumu na kuainisha

iwapo kazi hiyo imefaulu au haijafaulu. Kwa maoni ya mtafiti ni maarifa ambayo mtu yeyote anapaswa kuwa nayo ili aweze kuyatumia katika kufanya uchambuzi wa kazi fulani.Katika utafiti huu tumetumia nadharia ya Ufeministi katika kuchambua taswira ya mwanamke ndani ya *Diwani ya Midulu*.

### 2.6.1 Nadharia ya Ufeministi

Kwa mujibu wa Barrett (1988) ufeministi ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbalimbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopinga mfumo dume na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii ambazo zinazotawaliwa na wanaume.

Evance (1995) anaeleza kuwa nadharia ya kifeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1792 huko Ulaya, hususan katika nchi za Uingereza na Marekani. Katika kipindi hicho wanawake hawakuthaminiwa katika jamii zao na walikuwa ni watu waliokuwa katika daraja la chini. Vilevile, wanawake hawakuhusishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile kupiga kura au kuchaguliwa katika uongozi. Sehemu iliyoonekana hasa kuwafaa wanawake ni katika shughuli za jikoni. Unyanyasaji huu wa wanawake ndio uliopelekea kuibuka kwa nadharia hii ya kifeministi.

Nadharia ya kifeministi ilianza kuzungumzwa katika karne ya 19 na kutia fora miaka ya 1960 na 1970. Katika wakati huu wamagharibi walianza kuzungumzia matatizo yao katika machapisho na kufichua matatizo yanayowapata kama tabaka la kiuchumi na pia kama wanawake (Tong, 1989). Wamitila (2002) anaeleza kuwa baadhi ya kazi

za mwanzo kuyafafanua masuala ya wanawake kinadharia ni *A Vindization of the right of a woman* (1792) ya Mary Wollstonecraft. Pia kazi nyingine ni *The Second Sex* (1952) ya Simone de Beauvior ambaye alikosoa na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha au kumdunisha mwanamke, kama vile dini, ndoa na utamaduni. Kwa mujibu wa Wamitila, Simone de Beauvior anaeleza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Baada ya kukubali hali hiyo, mwanamke anaishia kuwa chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni huo. Mfano, ndoa ni asasi mojawapo ya kiutamaduni inayoendeleza ukandamizaji wa wanawake ambayo inamjenga kwenye imani na uwezo mkubwa alionao mwanaume na kuishia kumuangalia mwanamke kama chombo tu.

Wamitila (2002) anandelea kueleza kuwa uhakiki wa kifeministi wa Kimarekani unahusishwa na kazi ya Mary Ellman, *Thinking about Woman*. Dhamira ya kimsingi ya mwandishi huyu ilikuwa ni kuangaza jinsi wanawake walivyosawiriwa kwa namna mbali mbali katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Mwandishi huyu alimulika pia jinsi baadhi ya waandishi wa kike walivyouendeleza usawiri huo hasi wa wanawake katika kazi zao. Hali hii ilitokana na wao kukulia kwenye jamii zilizotawaliwa na itikadi ya kiume au “ubabedume” na kuishia kufyonza baadhi ya mitazamo kumhusu mwanamke ambayo inaakisiwa kwenye kazi zao.

Ntarangwi (2004) anasema kuwa nadharia ya kifeministi ni siasa kutokana na ukweli kwamba inaelekeza kubadili uhusiano uliopo kati ya wanaume na wanawake.

Uhusiano ambao umeranda katika nyanda nyingi za maisha kama vile familia, elimu, kazi, siasa, utamaduni na hata mambo ya starehe na anasa. Hivyo basi, ni nadharia inayotaka kuelekeza wanajamii namna ya kuishi, kutenda, na jinsi watakavyokuwa siku za usoni.

Kwa upande wa fasihi Ntarangwi (keshatajwa) anasema kuwa nadharia ya ufeministi imekuja kwa azma ya kusoma upya kazi za fasihi ili kusisitiza vipengele vilivyopuuzwa na wahakiki wengi ambavyo hawangeviona kwa sababu walikuwa wanafanya kazi katika nadharia za kijadi zilizomtukuza mwanaume.

Ntaragwi (2004) anaeleza kuwa baadhi ya mambo yanayozungumzwa na muungano huu ni kuunda upya uhalisia wa mwanamke kwa kupanga na kudhihirisha miundo ya kijadi ambayo inamtukuza mwanaume na kumkandamiza mwanamke. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) nadharia ya kifeministi inaongozwa na misingi kadhaa, nayo ni kutumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali ya mwanamke, kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na kupigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu. Misingi mingine ni kuhamasisha utungaji wa kazi za kisanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa ambao hawategemei wanaume ili wajulikane, huzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na huvumbua na kuziweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake.

Kwa upande wetu mtafiti ameamua kutumia nadharia hii katika kuongoza utafiti huu kwa sababu imesaidia kutuonesha jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika mashairi

ya *Diwani ya Midulu*. Hivyo, nadharia ya ufeminist ndiyo iliyoongoza utafiti huu kwa sababu inazungumzia masuala yanayowahusu wanawake na namna ya kutatua matatitzo yanayowakwamisha katika harakati za ukombozi. Aidha ni nadharia inayotoa mbinu mpya ambazo zina lengo la kumkuza mhusika wa kike.

Hata hivyo, nadharia ya ufeministi inaonekana kuwa na mapungufu kama vile, haielekei kuonesha au kuonekana kama ni nadharia moja kutokana na kufumbata mitazamo tofauti ya wananadharia wenye mawazo tofauti. Kwa mfano, Wafeministi wa Kimagharibi mjadala wao ni kupinga mfumo dume na wanaume kwa ujumla kwa mfano, katika masula ya mapenzi, sanaa na sehemu nyinginezo. Wakati wafeministi wa Kiafrika mjadala wao ni upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake kama ndoa za mapema, ukeketwaji, na mingineyo. Vilevile ni nadharia tegemezi kutokana na kuendelea kuchukua au kukopa mawazo kutoka katika mikabala mengine ya uhakiki kama Umarks, Saikochanganuzi, Semiotiki, Udenguzi na Hemenitiki.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia ambapo kazi zilizopitiwa ni zile zinazohusiana na dhana ya ushairi wa Kiswahili, taswira ya mwanamke katika mashairi ya Kiswahili na kazi tangulizi kuhusu mashairi ya Tigiti Sengo. Kazi hizi tangulizi zinaonesha kuwa hakuna mtafiti hata mmoja ambaye amechunguza taswira ya mwanamke katika kazi ya Tigiti Sengo ya *Diwani ya Midulu*. Pia, katika sura hii tumeelezea nadharia ya Ufeministi kuwa ndiyo iliyotumika katika kuchambua data za utafiti. Nadharia hii imetoa msaada

mkubwa katika kuhakikisha kwamba data za utafiti huu zimechambuliwa kwa ufanisi.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeeleza mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti. Mbinu za utafiti ni jumla ya mambo yote yanayohusiana na taratibu za kukusanya na kuchambua data kisayansi na kitaaluma (Babbie, 1999). Vipengele vilivyowasilishwa katika sura hii ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, aina ya utafiti, watafitiwa, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data na maadili ya utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo data za utafiti zilipokusanyiwa na pengine hata pale zilipochambuliwa (Cresswell, 2009). Eneo la utafiti huu ni Dar es Salaam na Zanzibar ambako hasa data za utafiti huu ambazo kwa asilimia zaidi ya tisini zilikusanywa kutoka katika maktaba zilizopo katika maeneo haya. Data za utafiti huu zilikusanywa maktabani ambapo maktaba zilizotumika ni maktaba ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, maktaba ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na maktaba kuu ya Taifa.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Utafiti wetu huu ni maktabani ambapo tulikusanya data za msingi kutoka katika *Diwani ya Midulu*. Utafiti wa maktabani ni ule unaofanywa na mtafiti kuingia maktaba na kusoma kazi aliyoiteua kwa kina ili aweze kupata data anazozihitaji

kulingana na malengo yake ya utafiti (Robson, 2007). Hivyo, ili kuweza kupata data za utafiti huu mtafiti pamoja na msaidizi wake waliingia katika maktaba tajwa hapo juu na kusoma diwani hizo mbili kwa kina na kudondoa baadhi ya mistari na beti za shairi ambazo zinaonekana kuwa zinaendana na madhumuni mahususi ya utafiti. Pamoja na kusoma diwani teule, pia, nyaraka mbalimbali zinazohusiana na data za utafiti zilipitiwa ili kuwezesha kupatikana kwa data za upili za utafiti wetu.

## 3.4 Watafitiwa

Watafitiwa katika utafiti huu ni *Diwani ya Midulu*. Kitafitiwa hiki kiliteuliwa kwa sababu ndicho kilichoweza kutupatia data ambazo tulizihitaji ili kujibu maswali ya utafiti wetu. Kutoka kwa kitafitiwa hiki tulipata data za msingi kuhusu ujitokezaji wa taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*.

## 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni sehemu ya jamii pana inayochukuliwa ili kuwa ni kiwakilishi cha jamii nzima iliyolengwa kufanyiwa utafiti (Babbie, 1999). Usampulishaji ni kitendo chenyewe cha kuchagua sampuli ambayo ndiyo hiyo sehemu ya jamii kuwa ni kiwakilishi cha jamii nzima. Sampuli ya utafiti wetu ni *Diwani ya Midulu* iliyoandikwa na Tigiti Shaaban Yusufu Sengo. Kazi hii tumeziteua kwa kutumia mbinu ya uteuzi inayojulikana kama usampulishaji lengwa. Usampulishaji lengwa ni mbinu ya kuteua sampuli ya utafiti kwa mtafiti kuteua sampuli yake kwa makusudi akiamini kuwa sampuli hiyo ilimwezesha kupata data anazozihitaji. Hivyo, kwa kutumia usampulishaji lengwa tumeweza kuteua *Diwani ya Midulu* ambayo ndiyo ilitoa data zilizowezesha kujibu maswali ya utafiti wetu.

### 3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa

Utafiti huu ulikusanya data za aina mbili ambazo ni data za msingi na upili.

#### 3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni aina ya data ambayo inakusanywa kwa mara ya kwanza na haijawahi kukusanywa data kama hiyo na mtafiti mwingine yeyote yule kwa minajili ya kutimiza malengo kama yanayokusudiwa kutimizwa katika utafiti huu (Kothari, 2008). Data za msingi ni data mpya na husaidia kupatikana kwa maarifa mapya ambayo hapo awali yalikuwa hayafahamiki kwa wanataaluma na jamii kwa jumla. Hivyo, data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika *Diwani ya Midulu*.

### 3.7 Data za Upili

Data za upili ni aina ya data ambazo tayari zimeshakusanywa na watafiti watangulizi na kuchapishwa katika majarida, vitabu, wavuti, tovuti, tasinifu na ripoti (Yin, 1994). Data za upili ni muhimu katika utafiti hasa katika kukazia maarifa mapya yaliyopatikana katika data za msingi. Hivyo, katika uchambuzi wa data za utafiti wetu tutatumia data za upili katika kushadadia hoja zetu na hatimaye kuimarisha sura ya nne ya tasinifu yetu.

### 3.8 Mbinu za Kukusanyia Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni usomaji makini na upitiaji wa nyaraka mbalimbali katika maktaba. Data za msingi zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini (Content Review) na data za

upili zilikusanywa kutokana na mbinu ya upitiaji wa nyaraka (Documentary Review).

### 3.8.1 Usomaji Makini

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kwa mtafiti kusoma kwa makini kazi za fasihi alizoziteua ili kuweza kupata data za utafiti wake na hatimaye kutimiza malengo ya utafiti wake (Young, 1984). Ili kuifanya mbinu ya usomaji makini kuwa ni yenye tija kwa mtafiti ni lazima mtafiti aainishe aina ya data anazozihitaji kutoka katika matini au kitabu anachosoma na kuandika katika daftari maalumu la kukusanyia data. Baada ya uainishaji wa aina ya data zinazohitajika ndipo sasa yeye pamoja na msaidizi wake wanaanza kusoma na kila watakapoona maneno, sentensi au aya inayoendana na aina ya data wanazozihitaji huchukua na kuandika katika daftari hilo maalumu walililoliandaa. Katika utafiti huu tulikusanya data kutoka katika *Diwani ya Midulu* kwa kusoma diwani hii kwa kina tena kwa kurudiarudia mpaka pale tulipoweza kupata data tulizozihitaji.

### 3.8.2 Upitiaji wa Nyaraka

Upitiaji wa Nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kutafuta kazi zinazohusiana na mada ya utafiti wake kwa lengo la kukusanya data ambazo zitatumika katika kujazilishia data za msingi (Yin, 1994). Kazi zinazohusiana na mada ya utafiti hupatikana katika maktaba zikiwa katika vitabu, makala, majarida, tasinifu, wavuti, tovuti na hata vipeperushi. Mtafiti wa utafiti huu alitafuta kazi hizo katika maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na katika maktaba za Chuo Kikuu

Huria Cha Tanzania kituo cha mkoa wa Tanga na Manyara. Data zilizokusanywa zilisaidia sana katika kuufanya utafiti wetu upate mwelekeo katika kuchambua data kwani tulipata muongozo juu ya namna watangulizi hao walivyochambua kazi zao.

### 3.9 Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huchambua data za utafiti wake kwa kuzitolea maelezo ambayo yanajibu maswali yake ya utafiti (Yin, 1994). Katika utafiti huu data ziliwasilishwa kwa kutumia njia ya madondoo ambapo mtafiti alidondoa baadhi ya beti na mistari ya mashairi ambayo alidhani kuwa ndani yake kuna data alizozihitaji.

Madondoo haya yaliwasilishwa chini ya mada kuu na ndogondogo ambazo zilikuwa zimebainishwa na mwandishi ili kuweza kujibu maswali ya utafiti na hatimaye kutimiza malengo ya utafiti. Kisha, madondoo hayo yaliyowasilishwa yalifanyiwa uchambuzi wa kina wa kimaelezo wenye kujibu maswali ya utafiti wetu. Maelezo katika uchambuzi wa data yalishadadiwa na hoja za nadharia ya Ufeministi ambapo taswira ya mwanamke katika mashairi ya Tigiti Sengo imebainishwa.

### 3.10 Hitimisho

Katika sura hii tumeelezea mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti. Vipengele vilivyowasilishwa ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, aina ya utafiti, watafitiwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanyia data na mbinu za uchambuzi wa data. Mbinu

hizi za utafiti zimesaidia kukamilika kwa hatua ya kukusanya data na hatimaye kuchambua data za utafiti.

## SURA YA NNE

## 4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

### 4.1 Utangulizi

Sura hii ya nne ya tasinifu hii inawasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kwa azma ya kutatua tatizo la utafiti huu. Mada ya utafiti huu ilikuwa ni Kuchunguza taswira ya Mwanamke katika *Diwani ya Midulu*. Ili kufanikisha mada hii utafiti uliweka malengo mahususi matatu ambayo yalikuwa ni kuhakiki taswira ya mwanamke katika mashairi ya Tigiti Sengo kama inavyosawiriwa katika *Diwani ya Midulu*, kubainisha sababu zinazofanya taswira ya mwanamke iwe hiyo inayosawiriwa katika Diwani ya Midulu na kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumiwa na mwandishi katika kujenga taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*. Malengo mahususi haya ndiyo yaliyotumika katika kuchambua data za utafiti ambapo lengo mahususi la kwanza limeunganishwa na la pili kutokana na ukaribu wake wa kimantiki. Lengo mahususi la tatu limewasilishwa peke yake na ndio la mwisho katika uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Uchambuzi wa data umefanywa kwa kuzingatia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Kifeministi.

### 4.2 Taswira ya Mwanamke katika Diwani ya Midulu

Lengo mahususi la kwanza katika utafiti huu lilikuwa linalenga kuhakiki taswira ya mwanamke kama inavyojitokeza katika Diwani ya Midulu. Kimsingi, tunapozungumza juu ya taswira ya mwanamke tuna maana kwamba ni namna au jinsi mwanamke anavyotazamwa, anavyochorwa au kutathminiwa na mwandishi

katika kazi za fasihi simulizi na andishi. Mwanamke amekuwa akitazamwa na waandishi wa kazi za fasihi kwa taswira mbalimbali ambazo nyingine ni chanya na hasi kulingana na mazingira na hali halisi ya maisha inayomzunguka mwandishi huyo. Mwanamke kama ilivyo kwa wanajamii wengine anasawiriwa katika hali tofautitofauti kama vile mlezi, mchapakazi, mwadilifu, mtafuta elimu, mshauri mzuri kwa jamii, kiumbe ambaye ni mbeya, malaya, mfitinishaji na kadhalika. Usawiri huu unatokana na maisha anayoishi mwanamke katika jamii yake na mambo anayoyafanya kila siku. Usawiri wa aina hii wa mwanamke unajitokeza pia katika *Diwani ya Midulu* ya mtunzi Tigiti Sengo kama inavyowasilishwa katika sehemu inayofuata.

### 4.2.1 Mwanamke Kiumbe Mlezi

Ulezi ni moja kati ya majukumu makubwa aliyonayo mwanamke si wa leo tu bali tangu enzi na enzi. Tangu kuumbwa mwanadamu mwanamke amekuwa ni kiumbe wa kulea watoto na hata waume zao katika familia (Evance, 1995). Si hivyo tu, bali pia mwanamke amekuwa ni kiumbe wa kulea wazazi wake, wazazi wa mume, ndugu wa pande zote wakiwemo mawifi, mashemegi na mashangazi wa mumewe. Malezi haya yanajumuisha kuwapikia chakula, kuwafulia nguo na kuwafanyia usafi mahali pa kulala na kupumzika. Mwanamke hufanya kazi hizi kwa moyo mmoja bila hata kusita bila malipo yoyote na wakati mwingine huishia kutukanwa au kusemwa kwa kauli ambazo si nzuri zisizo za shukurani wala asante (Koda, 2000). Katika kuonesha kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye hufanya malezi si kwa watoto wake pekee bali pia kwa wazazi, Tigiti Sengo katika Shairi lake la *Binti Yangu Khadija* (uk. 83) anasema:

*Mngu kanipa hidaya, Binti yangu Khadija*
*Hunilea kwa bembeya, kwao ndiko nenda hija*
*Mumewe ni mleya, mlezi wa twenye haja*
*Binti yangu Khadija, Mwenyezi takulipiya.*

*Sisikize ya duniya walimwengu zao hoja*
*Wapi amemzaliya, nia zao kutufuja*
*Na kututwa kumwambiya, yasiyokuwa ya haja*
*Binti yangu Khadija, Mwenyezi takulipiya.*

*Sisi hatumchi mtu, bali Muungu mmoja*
*Hatuna kilichochetu, ulezi si wa tunguja*
*Ramadhani mwanakwetu, si mtu wa kutondoja*
*Binti yangu Khadija, Mwenyezi Takulipiya.*

*Mshiketo muumeo, kitunze kidume chako*
*Wewe ndiwe tegemeo, maleziyo rehemako*
*Kusiwe na mregeo, subiri hadi mauko*
*Duniya mara haiko, Mola wetu egemeo*
*Binti yangu Khadija!*

Beti hizi za shairi zinaonyesha kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye hutoa malezi mazuri kwa wazazi kiasi cha kupatiwa sifa kemkem pamoja na kuombewa dua nzuri kwa Mwenyezi Mungu kuwa atapata ijara njema. Malezi anayoyatoa mwanamke yanafananishwa na bembea pale mtunzi anaposema, "hunilea kwa bembeya, kwao ndiko nenda hija." Bembea ni chombo au kifaa kinachotumika kumstarehesha mtu kwa kumpeleka mbele juu na kisha chini juu na kurudiwa hivyo mara kadhaa. Kitendo hiki huweza kufanywa na mtu mwenyewe au kufanyiwa na mtu mwingine. Starehe hii hutumiwa sana na watoto hasa wanapokuwa shuleni au katika michezo yao wawapo majumbani. Hivyo, malezi yanayoelezwa kuwa yanatolewa na binti Khadija kwa wazee wake ni mazuri yasiyokuwa na kifani. Ni malezi ambayo yanaonesha kuwa binti huyo si mtu wa kulalamika kwani wazee ni wasumbufu kutokana na hali yao na hivyo huhitaji subira na uvumilivu wa hali ya juu katika kuwalea vinginevyo mlezi anaweza kuchoka na hata kuamua kuacha kuwalea wazee.

Hata hivyo, Binti Khadija hakuwa hivyo bali alikuwa ni mtu mvumilivu wa hali ya juu ndio maana hata mzee mwenyewe anayasifu malezi ya Khadija. Kimsingi, hii ndio sifa ya wanawake wengi katika jamii kwani hujitoa sana katika malezi ya wanajamii bila kutarajia malipo wala shukurani (Khatib, 1985).

Katika ubeti wa pili tunapata ujumbe kwamba mzee huyo aliyekuwa akilelewa na binti Khadija hakuwa mzazi wa kumzaa Khadija bali ni mtoto wa kufikia tu. Haya yanabainika pale anaposema, “sisikize ya duniya, walimwengu zao hoja, wapi amemzaliya, niya zao kutufuja.” Hii ni kauli inayonesha kwamba wapo baadhi ya watu wasiopenda kuona mtu ambaye si mzazi wa mtoto husika kulelewa na mtoto huyo na hivyo kuanza kufanya ufitini ili malezi hayo yasitishwe mara moja kwa mzee huyo. Hata hivyo, binti Khadija hakuwa ni mtu wa kusikiliza watu kwani aliendelea kumlea mzee huyo kama kawaida bila kuchoka wala kunung’unika. Sababu kubwa iliyomfanya Binti Khadija kuwa na moyo huo na kutosikiliza maneno ya watu ni kutokana na kumcha Mungu na kufuata mafundisho ya Mwenyezi Mungu. Katika ubeti wa tatu mtunzi anasema, “sisi hatumchi mtu, bali Muungu Mmoja.” Hii ni kauli inayoonyesha kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye anatoa malezi kwa jamii kwa sababu ya kutii amri ya Mungu ya kumtaka kuwa na upendo kwa watu wote bila ubaguzi wa aina yoyote (Tong, 1989).

Ubeti wa nne unaonyesha kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye humleya mumewe. Haya yanabainika pale mtunzi anaposema, “Mshiketo Muumeo, kitunze kidume chako, wewe ndiwe tegemeo, maleziwe rehemako.” Hii ni uthibitisho kwamba mwanamke ni kiumbe ambaye anayetegemewa kuwa ndiye mlezi wa kila mtu katika

familia na bila wasiwasi mwanamke anao uwezo mkubwa wa kutekeleza jukumu hili (Ntarangwi, 2004). Hata hivyo, kwa mtazamo wa nadharia ya Kifeministi wao wanaona kwamba kumfanya mwanamke kuwa ndiye mlezi wa jamii pana namna hiyo ni kumfanya mwanamke kuwa na majukumu mengi na kushindwa kufanya shughuli za uzalishaji mali ili ajiimarishe kiuchumi (Barret, 1988). Mwanamke anapokuwa akifanya shughuli kama hizi, mwanaume huwa katika shughuli za uzalishaji mali na kujiimarisha kiuchumi huku mwanamke akiendelea kuwa masikini. Hivyo, kwa mujibu wa nadharia ya Ufeministi mwanamke hatakiwi kufanya majukumu yote hayo bali afanye mambo ya kuzalisha mali ili awe na uwezo wa kiuchumi kama ilivyo kwa wanaume.

### 4.2.2 Mwanamke na Stara

Stara ni aina ya kivazi au vazi ambalo linazuwia maungo ya mwanadamu awe mwanamke au mwanaume ambayo kwa mujibu wa sheria za dini hayaruhusiwi kuwekwa wazi mbele za watu wasioruhusiwa kuona maungo hayo (Njozi, 1990). Kwa upande wa mafundisho ya dini ya Kiislamu ambayo ndiyo yanayorejelewa na Sengo katika *Diwani ya Midulu*, mwanaume anatakiwa kusitiri mwili wake kuanzia chini ya magoti mpaka katika kitovu. Maungo yaliyopo hapo katikati hayaruhusiwi kisheria kuonekana kwa watu wengine isipokuwa mke (Sengo, 2009). Kwa upande wa mwanamke, stara yake ni mwili mzima isipokuwa uso na vitanga vya mikono isipokuwa kwa mumewe tu ndipo anaweza kuacha wazi maungo yake yote (Khatib, 1985). Katika maisha ya leo ya jamii wapo wanawake ambao wanajisitiri na wapo wengine wengi ambao hawajisitiri licha ya kuwa ni Waislamu na wamepata mafunzo juu ya kujisitiri. Hali hii inasababishwa na maendeleo ya utandawazi katika jamii

ambapo watu hujifunza tamaduni mbalimbali duniani na kuona wanawake wa mataifa mengine wakivaa nguo zenye kuonesha maungo yao na wengine kuvaa nguo za wanaume. Hali hii huchukuliwa kama ni namna fulani ya kuonyesha usawa baina ya mwanamke na mwanaume. Tigiti Sengo katika shairi la "Kwa Umbile Umruri (uk.28)," anasema:

*Macho yamekuteua, kwa umbile ni mzuri*
*Kwa mavazi kujitowa, haibayo twaikiri*
*Mbekoni ukozaliwa, twasifu kwa ushauri*
*Kukubali ni khiyari, kutii ulikolelewa*

*Nakutazama machoni, cheo chako kuwa Duke*
*Sasa umo masomoni, tunu usipige teke*
*Ukiingiya kazini, acha kabisa makeke*
*Ukirudi nyumbani, siyache uwanajike*
*Kama jina ni Khadija, sitamani kuwa Ali*
*Hivyo ulivyo ni tija, usitake uthakili*
*Kama mumeo wewe hija, hurulaini wa kweli*
*Watakao udhalili, wanaitwa baradhuli.*

Katika shairi hili mtunzi ametumia lugha ya mafumbo kuelezea kwamba mwanamke ni kiumbe ambaye anatakiwa kujisitiri kwa kuvaa nguo ambazo zitasitiri mwili wake bila kuonesha maungo kwa watu wasioruhusiwa kimaadili ya kidini, kiserikali na kijamii. Katika ubeti wa kwanza kunaelezwa kuwa mwanamke ambaye huvaa nguo za kuficha maungo yake hupendeza na pia hupata heshima kutoka kwa wanajamii wote na hasa wanaume. Mtunzi anasema, "Kwa mavazi kujitowa, haibayo twaikiri." Hii ina maana kwamba mwanamke ambaye huvaa mavazi stahiki ya kike tena yenye kusitiri mwili wake huonekana kuwa ni mzuri zaidi kuliko yule ambaye hajajisitiri. Hata hivyo, kwa jamii ya leo mtazamo wa wengi ni kuwa mwanamke anapovaa nguo za kubana, fupi na zenye kuonesha maungo yake ndiye husemwa kuwa kapendeza na huonekana kuwa ni binti au mwanamke wa kisasa (Nguta, 2011). Mwanamke ambaye huvaa hijabu na kujisitiri kwa nguo pana huonekana kuwa si mwanamke wa

kisasa bali ni mtu aliyepitwa na wakati afananishwaye na wazee waliozaliwa zamani miaka ya 1947. Jambo hili la wanawake kusifiwa na wanaume kuwa wamependeza kutokana na kuvaa nguo za aina hiyo huwashawishi wanawake wengi kuvaa nguo hizo na baadhi yao kuonesha hata sehemu za ndani kabisa za miili yao.

Mtunzi anaendelea kumsawiri mwanamke kuwa ni kiumbe ambaye anapaswa kujisitiri maungo yake na hatakiwi hata siku moja kujifananisha au kujilinganisha na mwanaume katika suala la mavazi. Katika ubeti wa tatu hapo juu mtunzi anasema, “Kama jina ni Khadija, sitamani kuwa Ali,” akiwa na maana kuwa mwanamke hapaswi kuvaa nguo za kiume na kutokana na maumbile au maungo yake kuwa tofauti na ya wanaume. Wanawake ambao huvaa nguo za kiume kama vile suruali tena zile za kubana hufanya maumbile yao kujichora na kuwa kama vile wapo uchi. Kwa msingi huo mwanamke ni mtu wa kuvaa nguo pana ambazo hazimuoneshi maumbile yake ili pamoja na mambo mengine asiwatamanishe wanaume kiasi cha kuweza kukosewa adabu.

Kulingana na mawazo ya wananadharia ya Kifeministi wao huamini kuwa suala la mwanaume kumtamani mwanamke halitokani na nguo alizozivaa mwanamke huyo bali ni akili tu ya mtu namna alivyoizamisha katika matamanio (Tong, 1989). Hivyo, wao wanadai kuwa mwanamke achwe avae nguo za chaguo lake na kumlazimisha kuvaa nguo za aina fulani ni kumnyima uhuru wa kuishi maisha yake kwa raha mustarehe (Spelman, 1988). Hali hii ndiyo inayoendelea katika jamii ya leo na hivyo wanawake wengi leo hii wanavaa nguo za wanaume na hivyo kutokuwa na tofauti za kimavazi baina ya wawili hao.

Mavazi ya kiume kuvaliwa na wanawake ni jambo ambalo linamchukiza sana mwandishi wa *Diwani ya Midulu* na kulisemea katika mashairi yake mengi. Anaeleza kuwa kitendo cha mwanamke kuvaa mavazi ambayo si yake kinashusha thamani ya mwanamke na kumfanya aonekane asiye na thamani mbele za wanaume. Hii ni sawa na kusema kuwa mwanamke ambaye huvaa mavazi ya kiume hupoteza uanawake wake na kutazamwa kama mwanaume au mtu asiye na maadili katika jamii. Katika Shairi la "Kitumbua cha Tosini (uk. 77)" mtunzi anasema kuwa:

*Wauzani utosini, dadangu Bii Mwajuma*
*Changu mimi ki kawani, kwani ni mtu mzima*
*Miyoto ya Kiwalani, kupepea si kuzima*
*Kigoli hajawa mama, wauzani jalalani?*

*Cha thamani faraghani, kwa mtu aliye mwema*
*Viovu vi vichakani, misasa yachuna nyama*
*Bumunda alitakani, alitakaye afuma*
*Cha kutembezwa si chema, chajiuza cha kawani.*

*Ama pajani usoni, wasahau una baba*
*Hasa hasa wauzani, kilichozidi kibaba*
*Mbona kitoka thamani, huogopi huna toba*
*Ya hewani si mahaba, hata humuwoni soni.*

Shairi hili limejengwa kutokana na lugha ya mafumbo ambapo jina la shairi, "Kitumbua cha tosini," lina maana ya mwanamke kuvaa nguo ambazo zinachora sehemu yake ya uke na kuifanya ionekane bayana kwa watu ambao watamtazama. Katika hali ya kawaida mwanamke wa aina hiyo anafananishwa na mtu ambaye anafanya biashara kama asemavyo mtunzi, "wauzani utosini, dadaangu Bii Mwajuma." Kuvaa nguo za kiume kama suruali na kaptura kwa mwanamke ni sawa na mwanamke huyo kuchukuwa uke wake na kuuweka katika paji la uso ili kila mtu aweze kuuona. Katika hali ya kawaida hakuna mwanamke ambaye anaweza kuchukuwa uke wake na kuuweka katikati ya kichwa bali ni matumizi ya lugha ya

picha inayoashiria kwamba mwanamke huyo atakuwa ni mtu ambaye ameishusha thamani yake kwa kuvaa nguo ambazo si stahiki yake. Katika ubeti wa tatu anasema, “Ama pajani usoni, wasahau una baba.” Hakuna tofauti kati ya uso na paja kwani vyote viko nje jambo ambalo kimaadili haliruhusiwi mwanamke kuonesha mapaja yake hadharani.

Kuzingatia maadili ni jambo la msingi ambalo kila mwanajamii anatakiwa kufanya ili kuepusha jamii na balaa hasa magonjwa ya hatari yanayosababishwa na zinaa kama vile Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI (Sengo, 2009). Tabia ya wanawake kuvaa nguo ambazo zinamfanya wanaume wawatamani kimapenzi huchangia sana katika kukithiri kwa vitendo vya zinaa na hivyo kusababisha magonjwa hatari kuongezeka kwa wingi. Jamii isiyokuwa na mipaka juu ya nani avae mavazi gani na mavazi gani asivae haiwezi kuwa ni jamii bora yenye misingi mizuri ya maisha kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Katika hali ya kustaajabisha wapo wanawake ambao huvaa nguo ambazo huonesha maungo yao ya ndani mbele za watoto wao kitu ambacho kwa kweli ni kinyume kabisa na maadili ya jamii ya Watanzania na Afrika yote. Wanaufeministi wanapotetea uvaaji wa nguo wa aina hii ni lazima waelewe kuwa wanapotosha maadili ya jamii na huenda ikawa ni jambo la kawaida kuona mtu na mama yake au dada na kaka wakiwa na mahusiano ya kimapenzi kutokana na kutamanishana kupitia mavazi yasiyostahiki. Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa mwanamke ambaye anajisitiri vizuri maungo yake huheshimiwa na watu wa rika zote na daima hawezi kubughudhiwa, kukashifiwa wala kukosewa adabu (Sengo, 2009).

### 4.2.3 Mwanamke na Kazi

Katika jamii zote za Tanzania, Afrika na duniani kote mwanamke ni kiumbe ambaye anasifika kwa uhodari wa kufanya kazi za uzalishaji mali na zisizo za uzalishaji mali kwa kujituma tena kwa uadilifu mkubwa (Mirikau, 2011). Ilikuwa hapo kale ambapo mwanamke alikuwa ni kiumbe wa kufanya shughuli za nyumbani tu kama vile kufua nguo, kuosha vyombo, kusafisha nyumba, kulea watoto, kupika chakula, kumlea mume na kazi nyingine nyingi za aina hiyo ambazo si za uzalishaji mali. Baadhi ya wanawake wa kipindi hicho walijitahidi kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali kama kilimo na ufugaji lakini hawakuwa wanufaika wa shughuli hizo. Mazao yaliyopatikana kutokana na uzalishaji huo yalikuwa chini ya mamlaka ya uamuzi wa mwanaume na mwanamke aligawiwa sehemu kidogo ya faida ya uzalishaji huo na wakati mwingine hakupatiwa sehemu yoyote ya mali hiyo (Boserup, 1970).

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko makubwa ya nafasi ya mwanamke katika kufanya kazi ambapo tunaona wanawake makundi kwa makundi wakishiriki katika shughuli za uzalishaji mali kupitia ujasiriamali mgodomdogo wa kuuza vyakula, mapambo, nguo, bidhaa za sokoni na nyingine nyingi za aina hii. Katika Diwani ya Midulu kunajitokeza usawiri wa mwanamke na kazi kupitia shairi la “Bi Hasina Hazina (uk. 39-43).” Katika shairi hili mtunzi anasema:

*Mwenye hoteli ni wewe*
*Ukae usimulie*
*Nasaha nazo upewe*
*Bi Hasina Hazina*
*Ulipokubali hayo*
*Hijuwa unayo moyo*
*Na Aqili ndiyo hiyo*
*Bi Hasina Hazina*
*Nilikupapo maarifa*

*Hoteli kuzidi sifa*
*Pawe kama pana dhifa*
*Bi Hasina Hazina*

Katika beti hizo tatu hapo juu mwanamke anasawiriwa kuwa mmiliki wa hoteli akitajwa kwa jina la Bi Hasina. Hii inaonyesha kuwa mwanamke huyo alikuwa ni mjasiriamali akifanya shughuli ya kuzalisha mali kupitia huduma ya malazi na chakula katika hoteli yake. Mwanamke huyo ni mmoja kati ya wanawake wengi ambao wamejikwamua kifikra na kuona kwamba si busara kukaa nyumbani na kushughulia mambo ya nyumbani tu na kuamua kufanya kazi hiyo ya hoteli. Mtunzi anasema kuwa, "Mwenye hoteli ni wewe," akiwa na maana kuwa Bi Hasina ndiye mwenye hoteli hiyo. Katika ubeti huo wa kwanza inaonyeshwa kuwa ili mtu yeyote aweze kufanikiwa katika shughuli ya uzalishaji mali anayoifanya ni lazima awe wazi katika kuelezea changamoto zinazomkabili ili aweze kusaidiwa mawazo na fikra za kufanikiwa zaidi. Mtunzi anasema, "Ukae usimuliwe, nasaha nazo upewe," akiwa na maana kuwa mjasiriamali yeyote yule akipatiwa maelekezo na ushauri juu ya kufanya shughuli zake kitaalamu zaidi ndipo anapoweza kufanikiwa. Katika ubeti wa tatu anasema, "nilikupapo maarifa, hoteli kuzidi sifa," hii ina maana kuwa baada ya kupatiwa ushauri mmiliki huyo wa hoteli alifanya maboresho na hoteli yake ikaendelea kupaa zaidi kwa kupata wateja wengi na kupata faida kubwa.

Kimsingi, suala la wanawake kufanya kazi za uzalishaji mali limesaidia mno katika kuongeza pato la familia na kuwezesha familia hizo kumudu gharama za maisha ambazo zinapanda kila siku (Ramadhani, 2013). Kwa mfano, familia nyingi zimeweza kulipa karo za shule za watoto wao kutokana na mama kujishughulisha

katika shughuli za uzalishaji mali. Familia nyingine hazina baba na hivyo mama hulazimika kufanya kazi kwa juhudi ili kupata kipato cha kuendeshea maisha ya familia yake. Aina hii ya maisha ndiyo inayopendekezwa na nadharia ya Ufeministi kwamba mwanamke ni lazima ajitume na apewe nafasi ya kufanya kazi ili asiwe tegemezi kwa mwanaume kwani upo uwezekano wa mwanaume kutokuwepo kutokana na sababu mbalimbali na maisha ya familia lazima yaendelee. Kwa mfano, inapotokea mwanaume ambaye ni baba wa familia amefariki na ndiye alikuwa akitegemewa kwa kila kitu katika familia hiyo itakuwa si uongo kusema kwamba familia hiyo sasa itayumba na kushindwa kumudu gharama za maisha. Hali kama hii ndiyo mara nyingine husababisha kuongezeka kwa watoto wa mitaani. Mwanamke kujishughulisha ni jambo muhimu ili aweze kuwa mkombozi wa familia yake pale baba wa familia anapokuwa hayupo (Nicolson, 1990).

Katika shairi hilo la "Bi Hasina Hazina," mwanamke hatajwi au haelezewi kuwa ni mfanyakazi za uzalishaji mali pekee bali pia anatajwa kama mtumishi wa shughuli za nyumbani. Mwanamke aliye makini hatakiwi kusahau majukumu yake ya nyumbani eti kwa sababu anafanya kazi fulani ya kumuingizia kipato kama Bi Hasina. Mwandishi wa *Diwani ya Midulu* katika shairi hilohilo la "Bi Hasina Hazina (uk. 39-43)," anaeleza kuwa:

*Wewe na muume wako*
*Kwake wewe ndiwe jiko*
*Na wewe kwake kijiko*
*Bi Hasina Hazina*
*Kaeni mfurahike*
*Ya umiya yafanyike*
*Magumu yavumilike*
*Bi Hasina Hazina*

Mtunzi anasisitiza kuwa, "wewe na muume wako, kwake wewe ndiwe jiko," akimtaka mwanamke kutambua wajibu wake kama mama katika familia licha ya kuwa yeye ni mjasiriamali au mtu mwenye kujishughulisha na kazi yoyote ile ya kiuchumi. Imekuwa ni jambo la kawaida hii leo wanawake walio wengi kuzama zaidi katika shughuli za uzalishaji mali na kusahau kabisa majukumu yao kama wanawake katika familia zao (Khalifa, 2013). Shughuli za nyumbani ambazo alitakiwa kuzifanya mama hivi sasa zimeachiwa mtumishi wa nyumbani anayefahamika kwa jina maarufu la "dada wa kazi." Kutokana na hali hii dada huyo wa kazi ndiye huachiwa kazi zote za nyumbani ikiwa ni pamoja na kutandika kitanda cha baba na mama, kumwandalia baba maji ya kukoga na taulo, kumwandalia baba nguo za kuvaa pamoja na viatu na mwisho kumwandalia kifungua kinywa. Hali hii huendelea kwa muda na mwisho wa yote dada wa kazi hugeuka na kuwa ndiye mama hapo nyumbani ambapo baba anashawishika kuwa na mahusiano ya kimapenzi na dada wa kazi na hatimaye hata kumpa ujauzito (Ntarangwi, 2004).

Kimsingi, harakati za ukombozi na usawa katika masuala ya jinsia ndiyo yaliyoifikisha jamii katika maisha ya namna hii ambapo mwanamke anadaiwa kuwa anaonelewa na mwanaume kwa kuachwa nyumbani na mwanaume kwenda kazini. Mwanamke naye anatakiwa kwenda kazini na shughuli za nyumbani atafutwe mtu mwingine ambaye ataajiriwa kuzifanya. Hapa ndipo dhana ya kuwa na dada wa kazi ilipoanza kushika kasi zaidi. Jambo hili si baya hata kidogo ila linakuwa baya pale mama wa familia anapomwachia kazi zote dada huyo wa kazi. Hivi leo hata maadili ya watoto yamekuwa ni changamoto kubwa ambapo watoto wadogo wanajihusisha katika mambo ambayo ni ya watu wazima na wengine kufanya vitendo vya uhalifu

(Sengo, 1987). Mathalani vitendo vinavyofanywa na watoto wanaojulikana kama “panya road,” katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya ni ishara ya mmomonyoko wa maadili uliosababishwa na watoto hao kukosa malezi ya baba na mama na hasa mama. Mwandishi wa *Diwani ya Midulu* kupitia mashairi yake anabainisha kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye nguvu na uwezo wa kuyamudu majukumu yote ikiwemo kufanya kazi za uzalishaji mali na pia shughuli za nyumbani. Hakuna shaka yoyote juu ya ukweli wa suala hili lakini changamoto ni kuwa muda wa kuweza kuyafanya hayo yote ndiyo unaokosekana.

### 4.2.4 Uzuri wa Mwanamke Tabia na Subira

Katika jamii kumekuwepo na mawazo yenye kukinzana juu ya uzuri wa mwanamke ni sura au tabia? Wapo wanaodai kuwa uzuri wa mwanamke ni tabia na wapo wanaodai kuwa uzuri wa mwanamke upo katika sura na maumbile ya mwanamke. Wanaume hufanya maamuzi ya kuowa au kutokuowa mtu kutokana na mojawapo kati ya uzuri wa sura na tabia. Mtaalamu wa fasihi ya Kiswahili Sengo (2009) anaeleza kuwa uzuri wa mwanamke ni tabia na sio sura kwani waliowa mwanamke kwa sababu ya uzuri wa sura yake leo hii wanalia msiba wa kujitakia. Mwanamke mwenye tabia nzuri ndiye awezaye kuilea familia na kuiwezesha kupata mafanikio katika maisha. Falsafa ya Sengo (2009) inajitokeza katika kitabu chake cha mashairi cha Diwani ya Midulu katika shairi la “Thamani ya Mke (uk. 58).” Katika shairi hilo anasema:

*Thamani ya mke, imejificha*
*Simwache apike, ule mchicha*
*Asome afike, akeshe kucha*
*Uzuri si shavu, rangi kupaka*
*Kutovisha mbavu, kheri ya paka*

*Na nywele za fuvu, ye kujivika*
*Tabiya ya nunu, yahitajika*
*Aso msununu, anapendeka*
*Mwenye fununu, tafurahika*
*Hunayo subira, nitakuwacha*
*Mke wa busara, hawi pakacha*
*Kukosa fikra, uwi m-bacha*
*Thamani mwanana, ni utiifu*
*Kuleya na wana, ni takusifu*
*Wewe tulizana, kwepa uchafu*

Beti za shairi hili zinatoa uthibitisho kuwa mwandishi wa *Diwani ya Midulu* anaamini kuwa uzuri wa mwanamke ni tabia na sio kujipodoa au kujipaka rangi. Ili kuweza kuifahamu tabia ya mwanamke ni lazima mtu afanye utafiti wa kutosha na sio kukurupuka. Mtunzi anasema, "thamani ya mke, imejificha," akiwa na maana kuwa kuifahamu tabia ya mwanamke ni jambo linalohitaji muda wa kutosha wa kufanya uchunguzi ili kujiridhisha kuwa mwanamke huyu ana tabia nzuri au mbaya. Mtunzi anasema, "uzuri si shavu, rangi kupaka," ikiwa na maana kuwa si jambo jema mwanaume kumuona tu mwanamke ambaye amejipodoa kwa vipodozi aina kwa aina na kudhani kuwa huyo ndiye mke mzuri wa kuowa na kuishi naye. Ndowa nyingi za siku hizi huvunjika haraka kutokana na waoaji kudanganywa na uzuri wa mwanamke aliyejipodoa kwa poda na lipustiki kuwa ndiye mwanamke mzuri wa kuowa na baada ya muda mambo huwa tofauti na alivyotaraji. Baada ya kutambua kuwa mkewe huyo si mwenye tabia nzuri hulazimika kumwacha na wakati mwingine wanakuwa tayari wameshapata watoto ambao hulazimika kuishi maisha yasiyokuwa na baba au mama. Watoto wenye bahati huweza kufanikiwa kuishi bila mzazi mmoja lakini wengi huishia kuwa na maisha magumu zaidi na wengine kuwa watoto wa mtaani.

Kimsingi, kutokana na hali halisi ya maisha ya leo upo uwezekano wa mwanamke ambaye ana tabia isiyosemeka kuificha tabia yake katika mwavuli wa kujiremba na kujipodoa ili aolewe na baada tu ya kuolewa tabia yake hujidhihirisha. Mtunzi anapendekeza kuwa mwanamke mzuri wa kumfanya kuwa mke ni yule mwenye tabia nzuri pamoja na subira. Maneno ya mtunzi kuhusu hili anasema, “Tabiya ya nunu, yahitajika, Hunayo subira, nitakuwacha.” Mwandishi anamsawiri mwanamke mwenye tabia nzuri na mwenye busara kuwa ndiye afaaye kuwa mke mwema na hivyo kuwasihi vijana na watu wote wanaokusudia kuowa kulitazama jambo hili kwa makini ili wasije wakapata matatizo hapo baadae. Maisha ya siku hizi ni magumu kwani hakuna uwezekano wa mtu kwenda kuomba mahitaji yake ya siku kwa jirani na kusaidiwa kila siku kwani hata jirani huyo naye pia maisha yake ni magumu. Mwanamke mvumilivu na mwenye subira ndiye anayetakiwa ili aishi kwa amani na mumewe hata pale mambo yao yanapokuwa si mazuri kifedha (Indede, 2011). Mtunzi anamalizia kwa kusema kuwa, “Thamani mwanana, ni utiifu,” akimaanisha kuwa mwanamke mtiifu ndiye mke mzuri na si sura wala umbo.

Sababu kubwa iliyomfanya mwandishi amsawiri mwanamke mwenye tabia nzuri na subira kuwa ndiye mke mwema ni kuwa hivi sasa ndowa nyingi hazidumu kutokana na waowaji na waolewaji kutokuwa makini katika kuchagua wenza. Asilimia nyingi ya waowaji na waolewaji hawajipi muda wa kutosha kuweza kufahamu vizuri tabia ya mhusika kabla ya kufanya maamuzi (Connell, 1987). Tunakubaliana na mawazo haya ya mtunzi kwa kiasi fulani lakini ukweli ni kuwa wapo pia wanaume ambao hawana tabia nzuri na wao kuwa ndio chanzo cha ndowa kuvunjika. Suala la kupata mke au mume mwema linahitajika kwa pande zote mbili yaani mwanamke na

mwanaume kujiridhisha kuwa anayetaka kumfanya kuwa mwenzi ni mtu mwenye tabia na maadili yanayokubalika katika jamii. Katika kutoa msisitizo mwandishi katika shairi la "Ndowa ina Mambo yake (uk.90-91)," anasema:

*Ndowa isimu mahaba, si jina bali ni chanzo*
*Msimamizi ni baba, muume mwenye mafunzo*
*Mke nyumbani akiba, ni sukani ya matunzo*
*Ndowa ina mambo yake, siri kuu ni subira*

Hivyo, subira ni kitu muhimu mno katika kuifanya ndowa iweze kudumu miaka yote ya uhai wa wanandowa kama ilivyokuwa kwa watu wa zamani. Watu wa zamani waliweza kukaa na wake zao katika kipindi chote cha uhai wao kwa sababu walijawa subira na uvumilivu.

### 4.2.5 Mwanamke na Uongozi

Tangu enzi na enzi imezoeleka kuwa kiongozi katika jamii ni mwanaume huku mwanamke akiwa muongozwaji katika kila jambo. Hali hii ilitokana na mfumo dume ambao ulimuona mwanaume ndiye mtu mwenye akili na maarifa mengi ya kufanya mambo kwa tija na ufanisi. Masuala yote yaliyohitaji kufanyiwa maamuzi katika ngazi ya familia yalifanywa na baba bila hata ya kumshirikisha mama kwa kuwa mama alihesabika kama mtekelezaji wa kile ambacho kitaamuliwa na baba (Koda, 2000). Mwanamke alichukuliwa kama mama wa nyumbani ambaye alistahili kufanya shughuli za jikoni kwa ukamilifu lakini zile za uongozi zikiwa mbali naye. Jambo hili liliwafanya hata wanawake wenyewe kuamini kuwa wao si watu wanaostahili kuwa viongozi bali mama wa nyumbani. Hata hivyo, wapiganiaji wa haki sawa za kijinsia ndio walioibua madai kuwa wanawake wanaweza kuwa

viongozi wakipewa nafasi hiyo. Wanaharakati hao walidai kuwa mwanamke anaweza kuwa kiongozi bora hata kuliko baadhi ya viongozi ambao ni wanaume.

Katika kipindi cha hivi karibuni serikali za mataifa mengi zimekuwa zikitowa nafasi za uongozi kwa wanawake kupitia uteuzi wa nafasi maalumu za uongozi katika bunge, serikali kuu, serikali za mitaa na mashirika ya umma (Ngaiza, 2002). Wengi kati ya wanawake hao waliobahatika kupata nafasi za uongozi wamekuwa watendaji waadilifu na wachapakazi hodari kuliko ilivyokuwa ikidhaniwa. Mtunzi wa *Diwani ya Midulu* ameliona suala hili na kulisawiri katika diwani yake hiyo ambapo ameonyesha kwamba mwanamke anaweza kuwa kiongozi mzuri na makini katika kufanikisha jambo. Katika shairi la “Mafundi Wangu Midulu (uk. 14-15),” anasema:

*Tangu wa kupimapima, Halfani na Hassani*
*Wa msingi kuuuma, na wendaji mchangani*
*Maweni waliyofuma, na Salum Ubenani*
*M’hulambili Bwana Juma, kwa Omari Kibaoni*
*Midulu mafundi wangu*
*Mzengile nyumba yangu*
*Nakushukuruni sana*

*Injini Mama Salama, kazi za Mwanamkulu*
*Ose onitanga Mama, wasaho tumbadikulu*
*Sadiki msaka nyama, mchimbaji wa sululu*
*Mjengaji wa kisima, mzuwanda tulu tulu*
*Midulu mafundi wangu*
*Mzengile nyumba yangu*
*Nawashukuruni sana*

Shairi hili linazungumzia habari ya ujenzi wa nyumba ya mtunzi huko kijijini kwake Midulu katika wilaya ya Bagamoyo mkoa wa Pwani. Katika ujenzi huo kulikuwa na mafundi tofautitofauti na Mama Salama alikuwa ndiye msimamizi wa ujenzi huo. Hii tunaisoma katika msitari wa kwanza wa ubeti wa pili kuwa, “Injini Mama

Salama, kazi za Mwanamkulu.” Kauli hii inadhihirisha kuwa mama Salama alikuwa ni kiongozi msimamizi katika shughuli hiyo ya ujenzi ambayo ilifanyika kwa ustadi uliokusudiwa. Injini ni chombo ambacho ndicho hufanya mitambo na magari kuweza kutembea na kufanya kazi iliyokusudiwa. Bila ya injini hakuna kinachoweza kufanyika katika viwanda vinavyotumia mashine zenye injini au magari na hivyo shughuli za usafirishaji kutofanyika. Kumbe basi, mama Salama ndiye aliyekuwa mwezeshaji wa shughuli zote za ujenzi wa nyumba hiyo tangu katika msingi mpaka ikakamilika.

Katika maisha ya siku hizi wanawake wanaonekana kuwa ni wasimamizi waadilifu wa miradi ya maendeleo, kazi za serikali na taasisi binafsi. Imekuwa si jambo la kawaida kusikia mtumishi fulani ambaye ni mwanamke amesimamishwa kazi kwa sababu ameshindwa kutimiza wajibu wake au amejihusisha na vitendo vya rushwa na ufisadi. Wahusika wakuu katika hili ni wanaume jambo linaloashiria kwamba baadhi ya viongozi wanaume si waadilifu katika nafasi za uongozi walizopatiwa (Nguta, 2011). Kitendo cha mama Salama kusimamia mradi wa ujenzi wa nyumba mpaka ukakamilika kinatoa uthibitisho kwamba wanawake wanaweza kuwa viongozi wazuri na kwamba wapatiwe nafasi za uongozi ili walete maendeleo katika nchi ya Tanzania.

Sababu kubwa iliyomfanya mtunzi kumsawiri mwanamke kama kiongozi ambaye anaweza kutimiza wajibu wake kwa ustadi na umakini ni kwamba kwa muda mrefu mwanamke amekuwa akitazamwa kama kiumbe wa jikoni ambaye hawezi kuwa kiongozi bora. Harakati za masuala ya kijinsia zimesaidia kuuthibitishia ulimwengu

kwamba mwanamke anaweza kuwa kiongozi mzuri kuliko hata mwanaume kama akipewa fursa. Kumbe sasa, ule mtazamo wa kwamba mwanamke hawezi kuwa kiongozi bora ndio umefungwa rasmi kutokana na uwezo mkubwa wa uongozi unaofanywa na viongozi wanawake duniani ambapo leo kuna Marais, wakuu wa mashirika ya Kimataifa, mawaziri, wabunge, wakuu wa mikoa, wakuu wa mashirika ya umma na binafsi, wakuu wa wilaya na magavana wa majimbo, wakurugenzi na wakuu wa taasisi. Hii inatoa wito kwa jamii nzima kuwa wanawake wapewe nafasi za uongozi kwa sababu wanaweza na wasinyimwe nafasi hizo kwa madai kuwa hawawezi kuwa viongozi bora.

#### 4.2.6 Mwanamke na Upendo

Mwanamke ni kiumbe ambaye ameumbwa na Mwenyezi Mungu na kupambwa kwa sifa ya upendo kwa watu wote wanaomzunguka kama vile mume, watoto, wazazi wa pande zote, mashemegi, mawifi na majirani (Kimmel, 1991). Upendo alionao mwanamke kwa watu wengine unasababishwa na ile hali ya kuwa ni mzazi anayebeba ujauzito kwa kipindi cha miezi tisa na baadaye kujifungua mtoto. Baada ya kujifungua humnyonyesha mtoto kwa muda wa miaka miwili na mtoto huyo huchukuwa miaka miwili mingine kuweza kucheza yaani kuanza kujitegemea. Baada ya kipindi cha miaka minne ndipo sasa mtoto anaweza kujitegemea na mama akapumua na kuwa huru kufanya mambo yake bila kuwa na wasiwasi juu ya mwanae. Mazingira haya ni moja kati ya mambo ambayo yanamfanya mama kuwa na upendo kwa wanadamu wote. Maelezo haya hayana maana kuwa wanaume hawana upendo kwa watu wengine lakini upendo wa mwanamke umezidia kiasi.

Mtunzi wa *Diwani ya Midulu* anathibitisha kwamba mwanamke ni kiumbe mwenye upendo kwa watu kutokana na matendo yanayofanywa na Mwajuma katika shairi la "Nakushukuru Mwajuma (uk. 07-08)," anaposema kuwa:

*Moyoni umenishiba, niwa kaka niwa ami*
*Kooni limekukaba, kwa huduma kunihami*
*Huli hadi ukashiba, kunikumbukiya mimi*
*Nakushukuru Mwajuma.*

*Ama binti ama ndugu, ulivyo umri wako*
*Huzili karanga njugu, kokote kule uliko*
*Utachota bagubagu, kutenga zangu na zako*
*Nakushukuru Mwajuma.*

*Mungu amekuteua, kipindi hiki cha dhiki*
*Ni vyakula kuletewa, shibe hainiondoki*
*Mtenda utatendewa, Takulipiya maliki*
*Nakushukuru Mwajuma.*

Beti hizi za shairi zinamsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye upendo uliopita mipaka kutokana na kuwajali watu wengine. Mtunzi anasema, "Huli hadi ukashiba, kunikumbukiya mimi," akionesha namna Mwajuma anavyowajali watu wengine kuliko kujijali yeye binafsi tu. Wakati amejaaliwa kupata riziki ya chakula na kuanza kula hujitahidi kukumbuka watu wengine ambao hawana chakula kuwa watakuwa katika hali gani na kuamua kwenda kuwasaidia. Mahali pengine mtunzi anasema, "Huzili karanga njugu, kokote kule uliko, utachota bagu bagu kutenga zangu na zako," ikiwa ni kauli inayotoa msisitizo juu ya upendo alionao Mwajuma kwa watu wengine katika jamii. Upendo wa mwanamke ni mpana mno na hauna mipaka ndio maana hata katika vita au machafuko mwanamke hawezi kukimbiya na kuwaacha nyuma watoto hata kama si wake wa kuzaa. Mfano mzuri ni ule unaonekana katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambapo makundi ya wanawake yanaonekana kuwa na mzigo mkubwa wa watoto ikilinganishwa na

makundi ya wanaume (Narizvi, 1982). Wanaume hukimbia peke yao kujiokoa na mashambulizi ya vita na kuwaacha akina mama wakiwa na watoto wao bila msaada. Kimsingi, katika maisha ya kila siku ndani ya jamii tumewaona wanawake wakiwa na upendo wa aina hiyo hata kwa waume zao na wanafamilia. Kwa mfano, mwanamke anaweza kwenda katika shughuli kama vile harusi, kipaimara, dhifa na nyinginezo na anaporudi nyumbani huleta zawadi ya vitu alivyokula katika sherehe na kuwapatia wanafamilia. Hii ni njia mojawapo ya kuonyesha kwamba mwanamke ni kiumbe mwenye upendo usiopimika. Wanaume walio wengi hawana upendo wa namna hii tena baadhi yao huingia katika vilabu vya pombe na kuagiza nyama choma, ndizi na chips bila hata kukumbuka kubeba kidogo kwa ajili ya wanafamilia yake. Kitu kibaya zaidi baadhi ya wanaume huwa hawaachi nyumbani fedha za matumizi za kutosha kutokana na kujijali wao wenyewe katika starehe za pombe na nyama choma.

### 4.3 Matumizi ya Fani katika Diwani ya Midulu

Lengo mahususi la tatu la utafiti huu lililenga kuchambua matumizi ya fani katika *Diwani ya Midulu* iliyotungwa na Tigiti Sengo. Fani ni moja kati ya vipengele vikuu vinavyounda kazi ya fasihi kama vile mashairi, riwaya, tamthiliya, maigizo, michezo ya watoto, vichekesho, nyimbo, misemo, vitendawili, misimu, methali na hadithi (Njogu na Chimerah, 1999). Kipengele hiki cha fani huelezwa kuwa ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia mwandishi katika kuiunda kazi yake iweze kuwavutia wasomaji au wasikilizaji pale kazi hiyo inapokuwa mbele yao. Fani huundwa na vipengele vidogovidogo ndani yake ambavyo huhusisha wahusika, muundo, mtindo, mandhari na matumizi ya lugha (Wamitila, 2008). Vipengele hivi vya fani hutumiwa na mtunzi

kwa namna ya kujengana na kukamilishana ili kuweza kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa na kwa namna iliyokusudiwa. Matumizi ya vipengele vya fani hutofautiana baina ya watunzi kulingana na uzoefu wao katika tanzu na vipera vya fasihi ya jamii husika. Katika *Diwani ya Midulu* kuna utajiri mkubwa wa matumizi ya fani yanayomfanya msomaji kutotamani kuiweka diwani hiyo chini pale anapoanza kuyasoma mashairi yaliyomo ndani ya diwani hiyo.

### 4.3.1 Kipengele cha Muundo katika Diwani ya Midulu

Muundo ni moja kati ya vipengele vya fani kinachojitokeza kwa upana zaidi katika mashairi ndani ya *Diwani ya Midulu*. Muundo unaelezwa kuwa ni mpangilio wa visa na matukio katika kazi za fasihi kwa utaratibu ambao unamwezesha msomaji kuelewa lengo kuu la mwandishi wa kazi hiyo. Katika taaluma ya ushairi, muundo hurejelea namna beti za shairi zilivyopangwa kwa kurejelea idadi ya mistari inayounda ubeti wa shairi husika. Katika *Diwani ya Midulu* kuna matumizi ya miundo tofauti lakini sisi tutajikita katika baadhi tu ya miundo ya mashairi ndani ya diwani hiyo ili kusaidia kukamilika kwa lengo mahususi la tatu la utafiti huu.

#### 4.2.1.1 Muundo wa Takhmisa

Takhmisa ni muundo wa mashairi ambapo ubeti mmoja wa shairi unakuwa na mistari au mishororo mitano (Massamba, 1983). Mwandishi Tigiti Sengo ametumia muundo huu katika mashairi kadhaa kwa lengo la kuwasilisha taswira ya mwanamke kwa wasomaji wa mashairi hayo. Mfano mzuri ni shairi la "Fitina zao za Bure (uk. 29)," kama linavyodondolewa:

*Shika nilokuwambiya, tukwa petu Mzuri*
*Kamata fuwatiliya, nafisiyo iwe nzuri*

*Khasira zako zuwiya, ibada ni kusubiri*
*Vita utajishindiya, utayapata ya kheri*
*Fitina zao za bure*

*Ukuu wako nyumbani, msikize mume wako*
*Kubwa sana wajibuni, kuzimudu kazi zako*
*Mtenzi huwa haneni, zuwiya malalamniko*
*Utapata amani, twakepa misukosuko*
*Fitina zao za bure*

Tumedondoa beti mbili tu za shairi hili ili kuonyesha namna muundo wa Takhmisa unavyojitokeza katika *Diwani ya Midulu*. Kwa kutumia muundo huu mtunzi ameweza kuwasilisha taswira ya mwanamke kuwa ni kiumbe anayetakiwa kumtii na kumheshimu mumewe na hatakiwi kusikiliza maneno ya wafitini kwani wanaweza kumharibia ndowa yake. Katika ubeti wa pili msitari wa kwanza mtunzi anasema, "Ukuu wako nyumbani, msikize mume wako," na mwishoni akimalizia na kibwagizo, "Fitina zao za bure." Kauli hizi zinamtaka mwanamke awe ni mtu asiyependa kusikiliza maneno ya watu na badala yake awe anamsikiliza mume wake tu ndio salama ya maisha yao itapatikana. Matumizi ya muundo wa takhmisa katika shairi hili yamesaidia kutoa ujumbe uliokamilika na kuwafanya wasomaji waelewe vizuri kile kilichosemwa katika shairi hilo. Aina nyingine ya muundo inayopatikana katika Diwani ya Midulu ni tarbiya kama unavyowasilishwa katika sehemu inayofuata.

#### 4.2.1.2 Muundo wa Tarbia

Tarbia ni muundo wa mashairi wenye mistari minne katika kila ubeti. Huu ni muundo mashuhuri kuliko miundo mingine kutokana na matumizi yake kuwa na nafasi kubwa kuliko aina nyingine za miundo katika utunzi wa mashairi (Mayoka, 1984). Baadhi ya watu huamini kuwa tarbia ndio muundo pekee wa mashairi ya

Kiswahili na shairi litakalokuwa na muundo tofauti na huu halitapewa nafasi kubwa ya kuwa shairi kama ilivyo kwa shairi la tarbia. Katika *Diwani ya Midulu* kuna matumizi ya miundo mbalimbali lakini muundo wa tarbia ndio uliotawala katika diwani nzima. Shairi la "Hidaya Binti Kinyanga (uk. 84-85)," ni mfano mzuri wa shairi lenye muundo wa tarbia kama linavyodondolewa baadhi ya beti zake:

*Nakushukuru Kinyanga, Hidaya binti Rashidi*
*Kumbukumbu kuzifuga, kwa maarifa na juhudi*
*Tangu siku za mafiga, Morogoro taradadi*
*Mahaba ya ki-Wadudi, hadi leo hujabwaga.*

*Ndowa zako kiza kiza, kizazi ukajaliwa*
*Kazini ulipendeza, nafasi ukazipewa*
*Ukizipata na jaza, kwa yetu kuhifadhiwa*
*Radhi zetu ukapewa, na ya Allah Muweza.*

Shairi hili limetumia muundo wa tarbia ambao umeelezea taswira ya mwanamke kuwa ni mtu mwenye upendo na mchapakazi kwa lugha toshelezi kwa msomaji kuelewa kile kinachoelezwa katika shairi hili. Kwanza kabisa anaelezewa Hidaya kuwa ni binti mwenye upendo wa dhati kwa watu tangu akiwa mtoto mpaka sasa mtu mzima. Mtunzi anasema, "Mahaba ya ki-wadudi, hadi leo hujabwaga," akitoa msisitizo kwamba binti huyo anayejulikana kwa jina la Hidaya ni mtu mwenye mapenzi yasiyokuwa na kifani. Hivyo, wanawake ni watu wenye upendo hata mahali fulani katika sura hii tulizungumzia suala hili. Mwanamke hatakiwi kuwa ni mwenye upendo kwa watu pale anapokuwa katika umri fulani na baada ya umri huo kupita basi anabadilika na kuwa si mtu mwenye upendo tena bali awe na upendo katika maisha yake yote.

Pia katika shairi hili mwanamke anasawiriwa kuwa ni kiumbe mchapakazi pale anaposema kuwa, "kazini ulipendeza, nafasi ukapatiwa." Hii ina maana kuwa

mwanamke huyo aliyejulikana kwa jina la Hidaya alikuwa hodari katika kufanya kazi mpaka akapewa cheo. Hii ni kawaida ya wanawake walio wengi kuwa ni wachapakazi na waadilifu zaidi kuliko hata baadhi ya wanaume.

Katika shairi la “Namshukuru Mwajuma (uk. 07-08),” pia kuna matumizi ya muundo wa tarbia katika beti zote tano za shairi hilo. Tumedondoa ubeti huu mmoa kuthibitisha hoja yetu kama ifuatavyo:

*Upate leo na kesho, Kwa mola nakuombeya*
*Usome ufike mwisho, vidato kuongezeya*
*Kisha ulipoze jasho, maisha kifurahiya*
*Nakushukuru Mwajuma.*

Ubeti huu wa shairi umeundwa kwa muundo wa mishororo minne inayomsisitiza Mwajuma kusoma mpaka aipate elimu ya juu kabisa katika jamii yake ili awasaidie wananchi wenzake katika harakati za kupambana na changamoto za maisha. Ilikuwa ni huko zamani ambapo wanawake walikuwa hawapelekwi shule kwa madai kuwa wao ni watu wa kuolewa tu na kuolewa hakuhitaji elimu yoyote ya shuleni bali mafunzo ya unyago na ya nyumbani yanatosha kumfanya mwanamke kuweza kuishi na mume. Mambo ni tofauti katika dunia ya leo ambapo watoto wa kike wanapelekwa shule na wanafanya vizuri katika masomo yao. Waswahili wanao msemo wao usemao, “ukimpatia mtoto wa kike elimu basi utakuwa umeipatia elimu jamii yote.” Ni wajibu wa kila familia kuhakikisha kuwa mtoto wa kike anapatiwa elimu ya kutosha ili baadae aweze kuielimisha jamii nzima itakayokuwa inamzunguka. Wanaharakati wa Kifeministi ndio wanaopigania katika kuhakikisha kuwa watoto wa kike wanapata haki sawa na wale wa kiume katika mambo mbalimbali ikwa ni pamoja na elimu (Nicolson, 1990).

#### 4.2.1.3 Muundo wa Tathilitha

Tathilitha ni muundo wa mashairi ambapo beti za mashairi hayo zina mishororo mitatu pamoja na kibwaigizo au msitari wa mwisho (Harris, 1962). Katika *Diwani ya Midulu* kuna mashairi kadhaa ambayo yametungwa kwa kuzingatia muundo wa Tathilitha na hapa tumetoa mfano wa shairi la "Thamani ya Mke (uk.58):

*Thamani ya mke, imejificha*
*Simwache apike, ule mchicha*
*Asome afike, akeshe kucha.*

*Uzuri si shavu, rangi kupaka*
*Kutovisha mbavu, kheri ya paka*
*Na nywele za fuvu, ye kujivika.*

*Tabiya ya nunu, yahitajika*
*Aso msununu, anapendeka*
*Mwenye fununu, tafurahika.*

*Hunayo subira, nitakuwacha*
*Mke wa busara, hawi pakacha*
*Kukosa fikra, uwi m-bacha.*

*Thamani mwanana, ni utiifu*
*Kuleya na wana, ni takusifu*
*Wewe tulizana, kwepa uchafu.*

Shairi hili lina beti tano zenye mistari mitatu mitatu kwa kila ubeti tangu wa kwanza mpaka wa mwisho. Muundo wa tathilitha uliotumiwa katika kuunda beti hizo umewezesha kutoa ujumbe uliokamilika kuhusu umuhimu wa mwanamke kuwa na tabia nzuri na subira dhidi ya maswahibu yote yatakayomsibu. Tabia nzuri, uvumilivu na subira ndivyo vitakavyomwezesha mwanamke kudumu katika ndoa yake (Barrett, 1988). Pia shairi hili linatoa angalizo kwa waoaji kuwa makini wakati wa kutafuta mwenzi wasije wakadhani kwamba uzuri wa mwanamke ni sura na

umbo badala ya tabia watajikuta wanaingia katika matatizo makubwa hapo baadae (Sengo, 1987).

Matumizi ya muundo katika *Diwani ya Midulu* ni ya aina kwa aina lakini katika utafiti wetu imetosha kuchambua aina tatu za miundo ambazo ni takhmisa, tarbia na tathilitha. Miundo hii kwa pamoja imesaidia kujenga taswira ya mwanamke katika mashairi tuliyoyatafiti kwa namna ambayo inamfanya msomaji kupata dhamira zilizokusudiwa huku akiburudika. Muundo wa tarbia ndio uliotawala katika mashairi mengi ikilinganishwa na miundo mingine. Sasa tutazame kipengele kingine cha kifani ambacho ni wahusika.

### 4.3.2 Wahusika katika Diwani ya Midulu

Wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mtunzi wa kazi ya fasihi kama chombo cha kubeba dhamira na ujumbe kwa lengo la kuufikisha kwa hadhira iliyokusudiwa (Senkoro, 2006). Wahusika wanaweza kuwa watu, wanyama, wadudu, vitu, mawe, miti, wanadamu, mazimwi, mashetani, majini na inatosha kusema kuwa wahusika wanaweza kuwa viumbe hai au viumbe visivyo na uhai. Dhana ya wahusika imezoeleka kusemwa kuwa inajitokeza zaidi katika hadithi, riwaya, maigizo na tamthiliya kuliko katika ushairi (Wamitila, 2008). Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kwamba si sahihi kudai kwamba katika mashairi hakuna matumizi ya wahusika kwa kuwa mashairi hata yale mafupimafupi kama ya Kezilahabi katika *Kichomi* (1974), *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008) yana matumizi makubwa ya wahusika. Mashairi yana matumizi ya wahusika wa aina zote kama ilivyoelezwa

hapo juu na wahusika hao ni nyenzo muhimu ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa.

Mtunzi wa *Diwani ya Midulu* ametumia wahusika wanadamu kwa kiasi kikubwa katika kujenga taswira ya mwanamke katika diwani yake. Mtunzi amemtumia mhusika Mwajuma katika mashairi kadhaa ndani ya diwani hii, lakini hapa tumetolea mfano shairi la "Jina la Mtu Huuwa (uk. 18)," kama lilivyodondolewa baadhi ya beti zake:

*Nilimwambiya Mwajuma, mamio ameishiwa*
*Na mimi siyayafuma, kazini sijagaiwa*
*Hicho ulichokichuma, fanya nawe kukigawa*
*Jina la mtu huuwa, hasa la mtu mzima.*

*Mwajuma hakuamini, neno aliloambiwa*
*Alidhani ni utani, mama leo achotewa*
*Kila kitu kighalani, kwa simu benki hupewa*
*Jina la mtu huuwa, kisa ukubwa ilani.*

*Mtu mkubwa hakosi, si mtu wa kukopewa*
*Hata hanayo mikosi, hivyo ndivyo adhaniwa*
*Mifukoni karatasi, madeni kurundikiwa*
*Jina la mtu huuwa, kumbe ukubwa nuksi.*

*Himwendeya na Debora, Mtolera kapasiwa*
*Mzee ana harara, dharura kutimiziwa*
*Aambiwe na Zahara, wote michango kutowa*
*Jina la mtu huuwa, kifanyiwa masikhara.*

*Hifika kwa Hikimani, shida yangu hiitowa*
*Haraka akaamini, tukaa tukapagawa*
*Punde akawa makini, alichonacho kugawa*
*Jina la mtu huuwa, asokosa ni manani.*

Katika shairi hili anatajwa Mwajuma kama mhusika juu ya kumpatia mama yake fedha ili akidhi mahitaji yake kwa kuwa baba alikuwa bado hajapata mshahara. Kitendo cha mhusika Mwajuma kuombwa atoe fedha kumpa mama kinaashiria kuwa

mwanamke ni mtu mwenye huruma na ni rahisi kusaidia wenye uhitaji au matatizo katika jamii. Mafunzo ya nadharia ya wanaufeministi inathibitisha kwamba mwanamke ni kiumbe mpole na mwenye huruma na yuko tayari kutoa msaada kwa mtu yeyote pale unapohitajika. Mwajuma anasawiriwa kutoamini kuwa ni kweli mama yake ana shida na hivyo kutotoa fedha na kudai Debora na Zahara nao waambiwe ili waweze kutoa fedha ambazo atapewa mama yao. Hata hivyo, Debora na Zahara nao hawakuweza kumsaidia mama yao mpaka pale Hikimani ambaye ni mwanaume alipotoa fedha za kumsaidia mama yao. Katika shairi hili, mtunzi anaonyesha kwamba matarajio yake hayakuwa sahihi kwani alidhani kuwa mwanamke ndiye mwenye huruma zaidi kuliko mwanaume katika kusaidia wenye shida lakini mambo yakawa ni kinyume. Uchambuzi huu unatufanya tuseme kuwa si wanawake wote ambao wana huruma ya kusaidia watu tena watu wa karibu kama inavyodhaniwa. Wapo baadhi ya wanawake ambao wamekosa huruma ya kike ya kujali na kuthamini watu wengine.

Matumizi mengine ya wahusika katika mashairi ya *Diwani ya Midulu* yanajitokeza katika shairi la “Pili Mulakifulago (uk.50),” ambapo mtunzi anasema:

*Aqili busara BAGO, Mungu alokujalia*
*Tangiya wetu udogo, darasani tukingiya*
*Tukitafuna mihogo, gulu tukitowezeya*
*Beti ninakutungiya, Pili Mulakifulago*
*Tulipofika nyumbani, kwako tukapiga hodi*
*Ukawa u furahani, ikakutoka baridi*
*Ulikumbuka zamani, kusoma hukufaidi*
*Jadi ilikufisidi, mara kitiwa ndowani*

Katika beti hizi mbili za shairi tajwa hapo juu tunafahamishwa mhusika anayejulikana kwa jina la pili. Mhusika huyu anaswiriwa kuwa ni mama aliyekuwa

na uwezo mkubwa katika masomo wakati akisoma shule ya msingi lakini ndoto zake zilikatishwa njiani baada ya kuozwa akiwa mdogo. Maelezo na mafunzo ya nadharia ya Ufeministi yanathibitisha kwamba katika jamii za zamani na hata leo katika maeneo ya vijijini wapo baadhi ya wazazi ambao huwaoza watoto wadogo na kuwanyima haki yao ya msingi ya kupata elimu (Kimmel, 1991). Jambo hili ni baya na halipaswi kuvumiliwa kwa kuwa linachangia katika kurudisha nyuma maendeleo ya jamii. Tumesema mahali fulani kuwa, "ukimpatia mtoto wa kike elimu utakuwa umeipatia jamii nzima elimu." Kumnyima mtoto wa kike elimu ni kuinyima jamii nzima elimu. Sasa tutazame matumizi ya mtindo katika mashairi yaliyopo ndani ya *Diwani ya Midulu*.

### 4.3.3 Kipengele cha Mtindo katika Diwani ya Midulu

Mtindo ni moja kati ya vipengele vya fani kinachotumiwa na watunzi wa kazi za fasihi katika kuwasilisha ujumbe na dhamira kwa hadhira ya kazi husika. Mtindo huweza kufasiliwa kama jinsi au namna mtunzi anavyotunga kazi yake na kumfanya kuwa na upekee ikilinganishwa na utunzi wa waandishi wengine (Massamba, 1983). Ni sahihi kusema kwamba matumizi ya mtindo katika utunzi wa kazi za fasihi hutofautiana kutoka mtunzi mmoja na mwingine ingawa upo uwezekano wa mtunzi fulani kuiga mtindo kutoka mtunzi mwingine. Mtindo wa mtunzi hujitokeza kwa namna mbalimbali kama vile uteuzi wa lugha anayoitumia, matumizi ya kiitikio na kibwagizo katika shairi, kuchanganya mitindo katika mashairi, kuchanganya lugha sanifu na isiyokuwa sanifu, kuchanganya lugha za makabila na Kiswahili na kadhalika. Katika tasinifu hii hatutachambua mitindo yote hii bali michache tu ili kutimiza lengo mahususi la tatu la utafiti huu.

#### 4.2.1.4 Mtindo wa Lugha ya Kawaida

Mtunzi wa *Diwani ya Midulu* amejitahidi kutunga mengi kati ya mashairi yake kwa kutumia mtindo wa lugha ya kawaida kuweza kueleweka kwa wasomaji. Hii haina maana kuwa mtunzi hakutumia lugha ya mafumbo katika utunzi wake, bali lugha ya kawaida ndiyo iliyotawala zaidi na lengo likiwa kuufanya ujumbe uliopo katika mashairi yake kuifikia hadhira pana zaidi. Mfano wa matumizi ya mtindo wa lugha ya kawaida tunaupata katika shairi la "Jamillah Acha Khasira (uk. 70-71). Mtunzi anasema:

*Ujanani ulikuwa, mgomvi ilipobidi*
*Hukutaka kudhuriwa, ulipinga uhasidi*
*Kazini kuonelewa, kwa kupinga ufisadi*
*Na pale hujaolewa, ulikana ufisadi*
*Leo hii waelewa, Jamillah acha khasira,*
*Yusufali mlelewa, mkononi kakuliya.*

*Allah alikuteuwa, mwanangu kunileleya*
*Huna la kusimuliwa, kwani yote yaeleya*
*Leo fitina kutiwa, ubaya kuwajengeya,*
*Wawili kuwabaguwa, Jamillah acha khasira.*

Mtindo wa lugha iliyotumika katika shairi hili ni wa lugha ya kawaida inayoeleweka kwa urahisi kwa msomaji bila kutaka ufafanuzi kutoka kwa mtu mwingine. Lugha iliyotumika katika shairi hili inamsawiri mwanamke kupitia mhusika Jamillah kama mtu anayechukia ufisadi kwa nguvu zake zote. Pamoja na kuchukia ufisadi pia anachukia ufisidi. Ufisadi ni istilahi inayotumika ikiwa na maana ya mtu au kikundi cha watu kujihusisha katika vitendo vya rushwa, ufujali wa mali za umma na kujipatia kipato kwa njia ambazo si za halali. Ufisidi ni istilahi inayorejelea husda, wivu au ufitini unaoweza kufanywa ili kuwagombanisha watu wawili wanaopendana. Maelezo na mafunzo ya wana Ufeministi yanathibitisha kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye hapendi vitendo viovu kama rushwa ndio maana hata

si mara nyingi kusikia kiongozi mwanamke akituhumiwa kujihusisha na rushwa kubwa kama ilivyo kwa viongozi wanaume (Connell, 1987). Lakini kuhusu ufisidi na husda wanawake wanaoongoza zaidi kuliko wanaume. Wanaufeministi hawawezi kukubaliana na kauli hii lakini huo ndio ukweli kwani hata taarab ya mipasho ilianzishwa na wanawake na maudhui muhimu katika nyimbo hizo ni kupashana, kusutana, kudhihakiana, umbeya, wivu, husda na kadhalika.

#### 4.2.1.5 Matumizi ya Mtindo wa Kiitikio na Kibwagizo

Katika taaluma ya ushairi kiitikio ni kile ambacho kinajitokeza katika msitari wa mwisho wa ubeti wa shairi kwa kutofautiana katika kila ubeti. Ubeti wa kwanza wa shairi unakuwa na kiitikio chake na ubeti wa pili na kuendelea unakiwa na kiitikio tofauti. Kwa upande wa kibwagizo, nao ni mtindo wa utunzi wa mashairi ambapo msitari wa mwisho unafanana katika beti zote za shairi. Mitindo hii miwili hutumika katika mashairi kwa lengo la kutoa msisitizo juu ya dhamira ambayo mtunzi anataka hadhira yake iielewe na kuizingatia. Hata hivyo, kibwagizo kinakuwa na nguvu zaidi ya kusisitiza ujumbe kwa sababu kinajirudiarudia katika kila ubeti wa shairi tofauti na kiitikio ambacho kinajitokeza tofautitofauti katika kila ubeti.

Katika *Diwani ya Midulu* kuna matumizi ya Kiitikio na Kibwagizo katika mashairi yanayojitokeza katika diwani hii. Katika shairi la “Wanangu Wamekomaa (uk. 88),” kunajitokeza matumizi ya kiitikio kama tulivyodondoa badhi ya beti hapa chini:

*Wanangu mjikusanya, na kazi mkagawana*
*Mmefika hadi Kenya, nafsi zikiungana*
*Mmekataa kukenya, ya mzee mkasana*
*Makubwa mliyafanya, umoja wetu ufana*
*Wawili tahunyahunya, kwa wao ushirikina,*

*Kama wao siwo wana, hayo watayatapanya.*

*Bi. Shekha mkazangu, kuleya unakujuwa*
*Kufu kutoka kwa Mungu, na kwenu ulilelewa*
*Kiniona na matungu, kwa homa nalewalewa*
*Dawa yangu chunguchungu, kijigali kinaliwa*
*Mtakao roho yangu, kila mtu kapangiwa,*
*Kupata ni majaliwa, Mpaji Bwana Mungu.*

Hili ni shairi lenye beti saba lakini hapa tumeteua beti mbili tu ili kuonyesha namna mtindo wa kiitikio ulivyotumika katika shairi hilo. Kila ubeti katika shairi hili una jumla ya mistari sita na kila ubeti una kiitikio tofauti na ubeti mwingine. Katika ubeti wa kwanza kiitikio kinasomeka, "Kama wao si wana, haya watayatapanya," kikiwa ni kiitikio kinachotoa msisitizo kwa watoto kuzingatia mawaidha na mafunzo wanayopewa na wazazi wao ili waweze kuishi maisha mazuri hapo baadae. Huu ni msisitizo unaeleza kuwa kama kweli wao ni watoto lazima wasikilize wasia huo kutoka kwa wazazi. Katika ubeti wa pili anatajwa Bi. Shekha na kupewa sifa kuwa anajuwa kulea watoto. Mwishoni mwa ubeti huo kuna kiitikio, "kupata ni majaliwa, mpaji Bwana Mungu," kikitoa msisitizo kwamba, wapo baadhi ya watoto hatawaelekeza mazuri kwa nguvu kubwa daima hawabadiliki na huishia kuwa wenye roho mbaya na ufedhuli.

Katika shairi la "Ndowa Ina Mambo Yake (uk. 90-91)," kuna matumizi ya kiitikio ambayo yanakaribiana na kibwagizo lakini hatuwezi kukitwa ni kibwagizo kwa sababu kina tofauti ya maneno machache kutoka ubeti mmoja na mwingine. Baadhi ya beti za shairi hilo ni:

*Ndowa isimu mahaba, si jina bali ni chanzo*
*Msimamizi ni baba, muume mwenye mafunzo*
*Mke nyumbani akiba, ni sukani ya matunzo*
*Ndoa ina mambo yake, siri kuu ni subira.*

*Subira imejificha, kilichowazi mapenzi*
*Ndoa mfano pakacha, yataka sana kuenzi*
*Na ikiwa ni mchicha, kitoweche sicho panzi*
*Ndowa ina mambo yake, siri nyingine ni huba*
*Yanachaji na kuchuja, haya yamewekwa mbele*
*Chaja yake si ya kuja, ongopa kimbelembele*
*Mkimya ndi mfuja, taitunguwa kwa ndole*
*Ndoa ina mambo yake, siri ya tatu ni hikima*

Shairi hili linatoa msisitizo juu ya mambo ya msingi ambayo yanatakiwa kuzingatiwa ili kuifanya ndowa iweze kudumu. Msitari wa mwisho katika kila ubeti kati ya hizi mbili ndio unaotoa msisitizo huo ambapo kipande cha kwanza cha msitari huo kinafanana katika beti hizo huku kipande cha mwisho cha msitari kikitofautiana. Huu ni mmoja kati ya mtindo mzuri ambao husaidia kukazia na kuikuza dhamira iliyokusudiwa na mtunzi iweze kuifikia hadhira kwa namna iliyokusudiwa. Mistari ya mwisho katika beti hizo inasomeka hivi; katika ubeti wa kwanza, "Ndowa ina mambo yake, siri nyingine ni huba," katika ubeti wa pili, "Ndowa ina mambo yake, siri nyingine ni huba," na katika ubeti wa tatu, "Ndowa ina mambo yake, siri ya tatu ni hikima." Tofauti iliyopo baina ya mistari hiyo ni ndogo sana lakini bado hatuwezi kusema hiki ni kibwagizo bali tunakiita kuwa ni kiitikio kinachokaribia kuwa kibwagizo. Msisitizo unaotolewa na kiitikio cha aina hii ni tofauti kabisa na viitikio ambavyo vipo tofauti katika kila ubeti.

Matumizi ya Kibwagizo yanajitokeza katika shairi la "Maisha Mwalimu Tosha (uk. 119)," ambapo katika beti zake zote msitari wa mwisho unafanana. Tuone mfano wa beti chache za shairi hilo kama ifuatavyo:

*Kipere wasema jipu, macho hayaoni mbele*
*Wenda huifungi zipu, wajiweka mbelembele*
*Vingapi vilivyo topu, itazame mbelewele*
*Maisha mwalimu tosha*

*Kukata kucha huwezi, chuma utakata vipi*
*Haibayo hupendezi, hujuwi kuzawa kupi*
*Mamio ndiye mzazi, hata akiwa mfupi*
*Maisha mwalimu tosha*

*Asolelewa na mama, na mayaya wa kikwao*
*Maisha atainama, hataupata mng'ao*
*Atawasha akizima, hadhi yake msikwao*
*Maisha mwalimu tosha*

Shairi hili lina jumla ya beti 5 lakini hapa tumetolea mfano beti 3 tu ili kuonyesha namna kibwagizo kilivyotumika kutoa msisitizo juu ya nafasi ya mama katika malezi ya watoto. Shairi hili linajenga dhamira kuwa mama ni mtu muhimu katika kumfanya mtoto kuwa na malezi mazuri katika jamii na hivyo watoto wawasikilize wazazi wao. Sababu kubwa ya mtunzi kuandika shairi hili ni kuwa, watoto wa siku hizi wamekuwa hawawasikilizi wazazi wao kwa kuwaona wamepitwa na wakati. Hali hii imechangia kuporomoka kwa maadili katika jamii kiasi cha watoto wadogo tu ambao walitakiwa kuwa shuleni leo wamekuwa walevi wa gongo, bangi, mirungi, madawa ya kulevya, vibaka na wahalifu wa makosa ya jinai (Khatib, 1985). Mtunzi katika shairi lake anakuja na kibwagizo, "Maisha mwalimu tosha," akiwa na maana sawa na ile ya methali ya Kiswahili, "Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu." Kibwagizo hicho kimetumika kutoa msisitizo kwa watoto kusikiliza malezi, maongozi, mafunzo ya wazazi wao ili wasije kujikuta wanafunzwa na maisha kwa sababu maisha hayana huruma kama aliyonayo mama.

Matumizi ya mtindo wa kibwagizo yanajitokeza katika mashairi mengi ya Tigiti Sengo kupitia *Diwani ya Midulu*. Shairi la "Mipaka ya Kupendana (uk. 68-69) ni mfano mzuri wa matumizi ya Kibwagizo. Hebu tuone mfano wa beti chache za shairi hilo kama ifuatavyo:

*Ni haramu na halali, mipaka ya kupendana*
*Tusiwe na ndimi mbili, kama twathaminiyana*
*Leo lile kesho hili, vibaya kutendeyana.*
*Mipaka ya kupendana, keshaiweka Wakili.*

*Binti uliyemzaa, hamwezi kuandamana*
*Akishakuwa kifaa, mwendani wake ni nana*
*Simfanyie hadaa, denini awe dhamana*
*Mipaka ya kupendana, keshaiweka Wakili.*

*Mke huyu ni wa kwako, ni haramu kwa hiyana*
*Hata kama ni tambiko, haimo katika suna*
*Vyote vya watu si vyako, usifanye usununu*
*Mipaka ya kupendana, keshaiweka Wakili.*

Shairi hili linazungumzia juu ya mipaka ya kupenda ambapo baba anaonywa kuwa si halali yeye kumtamani binti yake na kuwa na uhusiano wa kimapenzi. Imekuwa ni jambo la kawaida katika maisha ya siku hizi kusikia baba kambaka mtoto wake wa kike na baadhi ya akina baba huwa na uhusiano kabisa wa kimapenzi na watoto wao wa kike. Mtunzi ametumia kibwagizo, “Mipaka ya kupendana, keshaiweka Wakili,” akiwa na maana kuwa Mwenyezi Mungu amekataza watu kuwa na uhusiano wa namna hiyo. Kauli hii imerudiwa katika kila ubeti wa shairi hilo.

Pia katika ubeti wa tatu tunaona mwanaume akionywa kuwa, “Mke huyu ni wa kwako, ni haramu kwa hiyana,” ikiwa na maana kuwa si jambo la halali mwanaume kumwingilia mkewe kinyume na maumbile. Ingawa mke ameolewa kwa kufuata taratibu zote za ndowa lakini mume haruhusiwi kumwingilia mkewe kinyume na maumbile. Hivyo, kibwagizo cha shairi hili kinatoa msisitizo kwamba kitendo hicho hakifai na ni kinyume na haki za binadamu hivyo kila mtu anatakiwa si tu kwamba asikifanye bali akichukie kabisa.

### 4.3.4 Matumizi ya Lugha ya Mafumbo

Miongoni mwa sifa muhimu za fasihi ya Kiswahili ni kutumia lugha ya mafumbo ambapo mtunzi hueleza jambo lakini hamaanishi jambo hilo bali jambo jingine kabisa. Senkoro (2006) anaeleza kuwa lugha ya mafumbo ni ile ambayo hutumiwa kueleza jambo kwa kulificha ili kumfanya msomaji ajipe muda wa kutafakari ili aweze kuelewa dhamira zilizopo katika kazi hiyo ya fasihi. Misemo, methali, nahau na vitendawili hutumia lugha ya mafumbo kiasi kwamba mtu anaweza kuwa anasemwa kupitia msemo fulani lakini asielewe kama yeye ndiye anayesemwa. Akina mama hununua kanga zilizoandikwa misemo fulani kwa lengo la kufumbiana wao kwa wao. Kwa mfano, unaweza kuona kanga imeandikwa, "asiyejuwa maana haambiwi maana," kauli hii ni fumbo kubwa kwa mtu na anayehisi kuwa ndiye afumbiwaye atachukuwa muda kujiuliza ni nini hasa kinaelezwa katika kauli hii. Katika nyimbo za taarab pia kuna matumizi makubwa ya lugha ya mafumbo itumikayo kwa lengo la wahusika kupashana, kusutana, kusemana, kushushuana, kushushana hadhi na kuoneana wivu.

Mtunzi wa *Diwani ya Midulu*, ni mmoja kati ya watunzi wa mashairi ya Kiswahili ambaye anatunga mashairi yake kwa kutumia lugha ya mafumbo. Katika shairi la "Vyanzo Vinne Vya UKIMWI (uk. 153)," kuna matumizi ya lugha mafumbo kama ifuatavyo:

*UKIMWI na saratani, magonjwa ya kundi moja*
*Vyanzo vya hapa nchini, kwa hakika ni vimoja*
*Wa kwanza keneza ndani, yeye akiwa mmoja*
*Hiyo ilikuwa hija, hasa watu wa chamani.*

*Ni pembe nne mraba, ya pili ya dhahabuni*
*Kumbe ni jike la baba, rukhsa watu wapeni*

*Hata na wala vibaba, mwisho wao mpakani*
*Wakubwa ndege ndengeni, chuki dhidi ya mahaba.*

*Pembe ya tatu khatari, mzazi wake buruda*
*Cha wizi hakisubiri, lilizawa la husuda*
*Kufisidi hakuhuri, kuu fasiki fasada*
*Lilizidi kwidakwida, ati lagawa futari.*

Beti hizi za shairi hapo juu zinaelezea chanzo kikubwa cha UKIMWI ni zinaa lakini hakuna mahali katika beti hizo ambapo zinaa inatajwa waziwazi. Matumizi ya lugha kama, "Pembe tatu ya khatari, mzazi wake buruda," ni lugha mafumbo inayoashiria mwanamke ambaye anakuwa na wapenzi zaidi ya mmoja. Kitendo cha mwanamke kuwa na wanaume zaidi ya mmoja ni hatari na ndicho huweza kusababisha maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Kati ya wanaume hao upo uwezekano kila mmoja naye akawa na uhusiano wa kingono na mwanamke mwingine, na huyo mwanamke naye anaye mwanaume mwingine na mzunguko unaendelea kama hivyo kiasi ambacho mmojawapo kati yao akiwa na Virisi Vya UKIMWI anaweza kuwaambukiza wote waliopo katika kundi hilo. Kwa msingi huo ni jambo la busara kila mwanajamii kuachana na uhusiano wa kingono na kundi kubwa la watu kiasi hicho bali kina mtu awe mwaminifu kwa mwenzake ili kujikinga na maambukizi ya UKIMWI.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kwa lengo la kukamilisha lengo kuu la utafiti ambalo lilikuwa ni kuchunguza taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu* ya mtunzi Tigiti Sengo. Katika lengo mahususi la kwanza tumefanikiwa kubainisha taswira ya mwanamke kuwa ni mwanamke

kiumbe mlezi, mwanamke na stara, mwanamke na kazi, uzuri wa mwanamke tabia na subira, mwanamke na uongozi na mwanamke na upendo. Katika lengo mahususi la pili ambalo lilihusu sababu za mwanamke kusawiriwa hivyo anavyosawiriwa ambapo tumebaini kuwa, mtunzi amemsawiri mwanamke hivyo kutokana na sababu za kidini tena dini ya Kiislamu. Lengo mahususi la tatu lilihusu matumizi ya mbinu za kisanaa katika mashairi ya *Diwani ya Midulu* ambapo tumebaini matumizi ya muundo, mtindo, wahusika na lugha ya mafumbo. Sura inayofuata inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumewasilisha muhtasari wa tasinifu yote kwa kuegemea katika malengo mahususi ya utafiti. Pia tumetoa hitimisho la utafiti mzima na mapendekezo ya utafiti wa baadae.

### 5.2 Muhtasari

Muhtasari wa utafiti huu umezingatia mambo muhimu yaliyojadiliwa na kuwasilishwa katika sura ya nne ya tasinifu kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa matatu ambayo ni Kubainisha taswira ya mwanamke katika mashairi ya Tigiti Sengo kupitia *Diwani ya Midulu*, Kuelezea sababu zilizofanya taswira ya mwanamke iwe hiyo inayosawiriwa katika *Diwani ya Midulu* na Kuchambua mbinu za kifani zilizotumiwa na mwandishi katika kujenga taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*.

#### 5.2.1 Taswira ya Mwanamke katika Diwani ya Midulu

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilitaka kufahamu mwanamke anasawiriwa vipi katika mashairi ya Tigiti Sengo kupitia *Diwani ya Midulu* ambapo tumefanikiwa kubainisha taswira kadhaa za mwanamke katika mashairi hayo. Mwanamke anasawiriwa kama kiumbe mlezi si kwa watoto tu bali hata wazazi na walezi. Shairi la, "Binti Yangu Khadija (uk. 83," linaeleza namna mwanamke alivyomkarimu katika kulea watu wakubwa ambao hata si wazazi wa kumzaa. Wanadamu wote katika maisha ya leo wanatakiwa kuwa na moyo wa huruma kwa watu wazima bila

kujali nasaba kwa kuwa mara nyingi watu wazima hupata taabu sana hata wanapokuwa katika harakati za kufuatilia huduma za afya hospitalini. Katika hospitali zetu nchini Tanzania, wahudumu wa afya kama manesi wengi wao ni wanawake hivyo wanatakiwa kuwa na moyo wa huruma kwa watu wazima kama wazee.

Vilevile, mwanamke amesawiriwa kama kiumbe ambaye anatakiwa kusitiri mwili wake ili asiache maumbile yake wazi kiasi cha kuwatamanisha au kuwakarahisha wanaume. Shairi la, "Kitumbua cha Tosini (uk. 77)," ndilo ambalo linaelezea namna wanawake wa siku hizi wanavyovyaa nguo ambazo zinawachora maumbile yao. Neno "kitumbua" limetumika kwa lugha ya mafumbo kumaanisha sehemu ya uke ya mwanamke kwamba anapovaa suruali ya kubana upo uwezekano wa sehemu hiyo ya mwili wake kujichora na kuonekana bayana mbele za watu. Kitendo hicho si chema kwani kinakaribisha uzinifu ambao huweza kusababisha kuongezeka kwa maambukizi ya UKIMWI.

Sambamba na hilo, mwanamke anasawiriwa kama kiumbe mchapakazi anayehangaika kutafuta kipato ambacho kitamsaidia yeye na famila yake. Shairi la, "Bi Hasina Hazina (uk. 39-43)," ndilo ambalo linaonyesha namna Bi Hasina alivyokuwa akichacharika na shughuli za kuuza chakula katika hoteli yake huko kisiwani Pemba. Huu ni mfano mzuri wa kuigwa kwani katika dunia ya leo si jambo jema kwa mwanamke kukaa nyumbani kusubiri baba aende kazini ndipo alete fedha za matumizi. Huu ulikuwa ni mtazamo wa kizamani na leo hii hauna nafasi ndio maana akina mama wengi wanajishughulisha katika shughuli ndogondogo.

Katika *Diwani ya Midulu*, mwanamke anasawiriwa kama kiongozi makini anayeweza kusimamia jambo likafanikiwa vizuri zaidi. Shairi la, "Mafundi Wangu Midulu (uk. 14-15)," linamsawiri mwanamke kama kiongozi jasiri katika kusimamia miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa nyumba tangu katika kuchimba msingi mpaka kukamilika kwa nyumba. Hapo zamani ilizoeleka kuwa mwanaume tu ndiye mwenye ujuzi na maarifa ya kuweza kusimamia mradi au jambo lolote lile ndipo lifanikiwe. Katika jamii ya leo, mwanamke ameonyesha mfano kwamba anaweza na hakuna kitu ambacho kinaweza kumzuia kuwa kiongozi mzuri katika usimamizi wa miradi.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe mwenye upendo wa dhati kwa watu wote katika jamii na hana ubaguzi. Pia mwanamke mzuri anayesawiriwa katika Diwani ya Midulu ni yule mwenye tabia nzuri na subira na sio sura wala umbo. Hivyo, waoaji wanaaswa kutazama sifa hizo kwa makini kabla hawajaoa ili wasije wakajikuta wanaishia kujuta baada ya maji kumwagika kwani huwa hayazoleki.

### 5.2.2 Sababu za Mwanamke Kusawiriwa Hivyo Alivyosawiriwa

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa mwanamke amesawiriwa katika hali chanya tu na hajasawiriwa katika hali hasi. Sababu kubwa iliyofanya mwanamke akasawiriwa katika hali hizo ambazo ni mwanamke kama kiumbe mlezi, mwanamke na stara, mwanamke na kazi, mwanamke na tabia nzuri na subira, mwanamke na uongozi na mwanamke na upendo ni imani ya dini ya mtunzi. Mtunzi wa diwani hii Tigiti Sengo anaamini kuwa kutaja mabaya ya mtu hadharani ni sawa na

kuhamasisha mambo hayo yafanywe na watu wengine. Ndio maana hata mtu akifariki haitakiwi kutaja mabaya yake bali hutajwa mambo mema tu. Hii ni falsafa ya dini inalenga katika kutokuhamasisha mambo maovu bali kuhamasisha mambo mema katika jamii. Mafundisho ya dini yanamtaka hata mtu binafsi kama akifanya jambo ovu asitangaze uovu huo kwa watu bali aufiche kwani kufanya hivyo husadikiwa kuwa ni kitendo kinachomuudhi sana Mwenyezi Mungu.

### 5.2.3 Matumizi ya Vipengele vya Kifani

Lengo mahususi la tatu la tasinifu hii lililenga kuchambua vipengele vya kifani vilivyotumiwa na mwandishi katika kujenga taswira ya mwanamke katika Diwani ya Midulu. Vipengele vya muundo, mtindo, wahusika na matumizi ya lugha ya kimafumbo ndivyo vilivyoibuliwa katika matokeo ya utafiti huu. Kwa upande wa muundo, imebainika kuwa mtunzi ametumia miundo ya aina tofautitofauti kama vile muundo wa takhmisa, tarbia na tathilitha. Hata hivyo muundo wa tarbia ndio uliotawala katika mashairi mengi ya mtunzi huyo. Kwa upande wa mtindo, pia ametumia mitindo ya aina kadhaa kama vile mtindo wa kutumia lugha ya kawaida na mtindo wa matumizi ya kiitikio na kibwagizo. Pia kuna matumizi ya wahusika na lugha ya mafumbo ambapo vipengele vyote hivi vimetumika katika kujenga taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu*.

## 5.3 Hitimisho

Kwa kiasi kikubwa mtunzi amemsawiri mwanamke katika nafasi chanya na hakuna nafasi hasi hata moja. Mahali fulani alitumia taswira hasi ya mwanamke kama kutolea mfano tu kwamba mwanamke hatakiwi kuwa hivi bali anatakiwa kuwa hivi.

Sababu kubwa iliyomfanya mtunzi amsawiri mwanamke katika hali hiyo ni kutokana na imani ya dini ya mtunzi kuwa haimruhusu kuelezea mabaya kwani atakuwa anabariki yaendelee kufanyika katika jamii. Hili ni jambo zuri lakini hata hivyo, katika maisha halisi ya jamii hakuna kiumbe ambaye ni mkamilifu aliyekuwa mwema tu asiyekuwa na upande wa maovu au mambo yasiyokubalika katika jamii. Kwa maoni yetu, tulidhani kwamba ingekuwa ni jambo jema kwa mtunzi kumsawiri mwanamke kama vile anavyotokea katika maisha ya kila siku kwa nia ya kuifundisha jamii juu ya mwenendo mwema wa maisha.

## 5.4 Mapendekezo

Katika utafiti huu tumeshughulikia taswira ya mwanamke katika *Diwani ya Midulu* pekee na hivyo tunapendekeza utafiti mithili ya huu ufanyike kwa kulinganisha taswira ya mwanamke kati ya *Diwani ya Midulu* na *Tungizi za Mnyagatwa* zote za Tigiti Sengo.

Vilevile, tunapendekeza utafiti kama huu ufanywe kwa kulinganisha na kulinganua taswira ya mwanamke katika mashairi ya Tigiti Sengo na mshairi mwingine yeyote wa mashairi ya Kiswahili.

# MAREJELEO

Alhabib, E. A. (2012), “Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Taarab, Tasinifu ya *M.A. Kiswahili*, CKHT.

Babbie, E. (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Barrett, M. (1988), *Women Oppression Today: The Marxist Feminist Encounter (Revied)* London: Verso.

Boserup, E. (1970), *Women’s Role in Economic Development*, New York: St. Martin’s Press.

Connell, R. W. (1995), *Musculinities*, Berkeley: University of Califonia.

Cresswell, J. W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Evans, J. (1995), *Feminist Theory Today: An Introduction to Second-Wave Feminism*, New Park, CA: Sage.

Frolova, N. (2003), “Euphrase Kezailahabi: The Renewal of Kiswahili Poetry. In *Kiswahili*, Vol. 66 Dar es salaam. IKR.

Harris, L. (1962), *Swahili Poetry*, London: OUP.

Indede, F. (2009), “Mwanamke Angali Tata katika Ushairi wa Kisasa?” katika *Swahili Forum* 18 (2011): 163-197.

Ismail, J. H. (2010), “Nafasi ya Nyimbo za Bongo Fleva katika Uelimishaji wa Haki katika Jamii”. Katika *Mulika.* Namba 29&30, Dar es Salaam: TATAKI.

Kezilahabi, E. (1974), *Kichomi,* Nairobi: Heinemann Educational Books.

Kezilahabi, E. (1976), *Shaaban Robert Mshairi*, Dar es Salaam: Heineman Educational Books.

Kezilahabi, E. (1988), *Karibu Ndani*, Dar es Salaam: DUP.

Kezilahabi, E. (2008), *Dhifa*, Nairobi: Vide-Muwa.

Khalifa, A. I. S. (2012), “Usawiri wa Masuala ya Kijinsia katika Lugha ya Mashairi. Mifano Kutoka Mashairi ya Bongo Fleva Tanzania”, Dar es Salaam. Tasnifu ya *M.A. Kiswahili*. CKHT.

Khalifani, M. Y. (2013), “Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Kandoro: Mifano kutoka Katika Mashairi Yake,” Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Khatib, M. (1985), “Utenzi wa Mwanakupona,” katika *Mulika* 7:46-52.

Kimmel, M. S. (1991), *Men Confront Pornography*, New York: Meridian.

Kitogo, S. A. (2002), “The Poets Contribution to Political Development: A case of Saadan Abdul Kandoro,” Unpublished *M.A. Thesis* UDSM.

Knappet, I. J. (1977), “The Appreciation of Kiswahili Poetry”. *In Kiswahili Vol. 44/2,* September, Dar es Salaam: IKR.

Kombo, O. M. (2014), “Kuchunguza Tamathali za Usemi katika Mashairi ya Magazetini: Uchunguzi Kifani wa Mashairi ya UKIMWI katika Magazeti ya Mzalendo, Nipashe, Majira, Uhuru na Mtanzania,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Kothari, C. R. (2008*), Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Mansour, A. A. H. (2013), “Kuchunguza Vipengele vya Fani katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganuzi na Ulinganishi wa Mashairi ya Euprase Kezilahabi na Haji Gora Haji”, Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Massamba, D. P. B. (1983), "Suala la Ushairi wa Kiswahili". Katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili-Fasihi namba 3. Dar es Salaam: TUKI.

Mayoka, J. (1984). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Nairobi: EALB.

Mirikau, S. A. (2011), "Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya za Wamitila K.W." Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulokozi, M. and Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH

Mulokozi, M. M. (1975). "Revolution and Reaction in Swahili Poetry". *In Kiswahili, Vol. 45/2*. Dar es Salaam: IKR, Kur. 46-65.

Mulokozi, M. M. (1996), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (2002), *The African Epic Controversy: Historical, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Poetry and Performance*. Dar es Salaam: IKR.

Mulokozi, M. M. na Sengo, T. S. Y. M. (1995). *History of Kiswahili Poetry* [AD 1000-2000]. Dar es Salaam: TUKI.

Narizvi, S. (1982), *The Sociology of the Life nature of Politics*. Austarilia: Edmund Burke.

Nguta, F. (2011), "Fani na Usawiri wa Wahusika katika Tamthiliya ya Pango na Mama ee," Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Njogu, K. na Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, JKF.

Njozi, H. (1990), “Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics,” *Kiswahili* 57: 55-67.

Ntarangwi, M. (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Rock Isaland: Augustine College.

Omari, S. (2008), “Mtindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania”, Katika *Kiswahili*, Juzuu 69. TUKI, Kur. 73-92.

Omari, S. (2009), “Tanzania Hip Hop as Popular Literature”, Unpublished PhD. *Thesis*, UDSM.

Omary, M. (2011), “Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008)”, Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Omary, M. (2015), “Kuchunguza Ufasihi Simulizi katika Kazi za Euphrase Kezilahabi: Mfano kutoka katika Vitabu vya Kichomi, Karibu Ndani na Dhifa,” Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Ramadhani, S. K. (2013), “Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee”. Tasinifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Robson, C. (2007), *How to do a research project: A guide for Undergraduate Students*, Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Safari, A. J. (2010), “Utangulizi katika *Diwani ya Midulu*,” Dar es Salaam: AERA.

Samwel, M. (2010), “Masuala ya Kisasa katika Mashairi ya Mapenzi ya Muziki wa Bongo fleva”, Katika *Mulika,* Na. 29&30. Dar es Salaam: TATAKI.

Sengo, T. S. Y. M. (1987), *Fasihi Simulizi, Sekondari na Vyuo*: Dar es Salaam: Nyanza Publications Agency.

Sengo, T. S. Y. M. (2009), *Sengo na Fasihi za Kinchi*, Dar es Salaam: AERA Publishers.

Sengo, T. S. Y. M. (2010), *Diwani ya Midulu*, Dar es Salaam: AERA Publishers.

Senkoro, F. E. M. K. (2006), "Fasihiya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi", katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Spelman, E. (1970), *Inessential Women: Problems of Exclusion in Feminist Thought*. Boston: Beacon Press.

Tong, R. (1989), *Ferminist Thought: A Comprehensive Introduction*. Boulder, CO: Westiew Press.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: PPL.

Wamitila, K. W. (2008), *Kanzi ya Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Yin, R. K. (1994), *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Enalewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.